# UKIUSHI KATIKA LUGHA YA KIMAONGEZI DHIDI YA KANUNI ZA KISWAHILI SANIFU

NA: SHAKE, ROSE MGHAMBI

TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA
'MASTER OF ARTS' KATIKA CHUO
KIKUU CHA NAIROBI.

University of NAIROBI Library
0369817 2

1991

# UNGAMO

"Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kutosheleza mahitaji ya shahada katika Chuo Kikuu kingine cho chote."

ROSE M. SHAKE

"Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii wa Chuo Kikuu"

DKT. JAY KITSAO

DKT. MOHAMED BAKARI

PROF. MOHAMED ABDULAZIZ

# T A B A R U K U

Tasnifu hii naitabarukia baba yangu mzazi, marehemu Bw. Samuel Shake, ambaye aliaga dunia mara tu kazi hii ilipokuwa inakamilika. Mwenyezi Mungu amuweke mahali pema peponi!

Pia,

Mamangu, Bi. Ruby Shake, ambaye, pamoja na marehemu babangu walihakikisha kwamba nimepata malezi mema.

YALIYOMO


YALIYOMO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . i

SHUKURANI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . iii

MUHTASARI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . v

SURA YA KWANZA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

1.0 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 1

1.1. SOMO LA UTAFITI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 5

1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU . . . . . . . . . . . . . . . . . 6

1.3 UPEO WA TASNIFU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 9

1.4 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO . . . . . . . . . . . . . . 10

1.5 HAIPOTHESIA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 12

1.6 YALIOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI . . . . . . . . . . . . 13

1.7 MISINGI YA NADHARIA . . . . . . . . . . . . . . . . . 14

1.8 NJIA ZA UTAFITI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 17

1.9 HITIMISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 25

SURA YA PILI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 27

2.0 LUGHA NA MATUMIZI YAKE KATIKA JAMII . . . . . . . . . 27

2.1 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 27

2.2 MASIALA MACHACHE KUHUSU MATUMIZI YA LUGHA . . . . . . 28

2.3. HALI YA LUGHA NCHINI KENYA (Muhtasari) . . . . . . . 31
2:3:1 LUGHA YA KISWAHILI MJINI NAIROBI . . . . . . . 34

2.4. KISWAHILI SANIFU . . . . . . . . . . . . . . . . . . 36

2.5 DHANA YA UKIUSHI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 38

TANBIHI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 43

SURA YA TATU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 44

3.0 UKIUSHI KATIKA MAONGEZI YA LUGHA YA KISWAHILI . . . . . 44

3.1 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 44
3.1.2 VIWANGO VYA UFASAHA WA LUGHA . . . . . . . . . 49

3.2 UKIUSHI KULINGANA NA KIWANGO CHA FONOLOJIA . . . . . . . 52

3.3 HITIMISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 71

SURA YA NNE . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 73

4.0. UKIUSHI WA KISARUFI . . . . . . . . . . . . . . . . . . 73

4.1 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 73
4.2 MAKOSA YA KIMOFOLOJIA NA KIMOFOFONEMIKI . . . . . . . . 74
4.2.1 MABADILIKO KATIKA NGELI: . . . . . . . . . . 74
4.2.2 KUZUSHA VIAMBISHI VISIVYOKUWEPO: . . . . . . . 76
4.2.3 MAKOSA KATIKA MNYAMBULIKO WA VITENZI . . . . 78

4.3 MAKOSA YA KISINTAKSIA . . . . . . . . . . . . . . . . . 83

4.4 HITIMISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 89

SURA YA TANO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 90

5.0 UKIUSHI WA KIMSAMIATI . . . . . . . . . . . . . . . . . 90

5.1 UTANGULIZI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 90

5.2 MISAMIATI ISIYOKUWA YA KISWAHILI . . . . . . . . . . . 91

5.3. MSAMIATI WA KISWAHILI AMBAO HAUKUTUMIKA KWA MAANA YAKE HALISI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 93

5.4. TAFSIRI ZA MOJA KWA MOJA KUTOKANA NA LUGHA ZA KWANZA . 96

5.5. HITIMISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 97

SURA YA SITA . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 99

6.0. HITIMISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 99

6.1. MAPENDEKEZO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 103

KIAMBATISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 105

MAREJEO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . 106

## SHUKURANI

Napenda kukishukuru chuo kikuu cha Nairobi kwa kunitunukia fursa ya kuweza kusomea masomo yangu ya digrii ya uzamili. Hasa Profesa Phillip Mbithi ambaye kutokana na ukarimu wake niliweza kugharimiwa masomo yangu na chuo kikuu.

Shukurani zangu pia ni kwa mwenyekiti wa Idara ya Ismu na Lugha za Kiafrika Bi. Lucia Omondi na wahadhiri wote wa idara hii kwa kunipa moyo wakati wa kuandika kazi hii na katika masomo yangu kwa jumla.

Natoa shukurani nyingi kwa wasimamizi wa kazi hii, Profesa Mohamed Abdulaziz, Dakta Jay Kitsao na Dakta Mohamed Bakari ambaye pia alinisaidia kuichagua mada hii.

Aidha, nawashukuru pia wanafunzi wenzangu Mutonya, Mc'Onyango, Murage, Yalwala na Likhako ambao kwa ushirikiano wao katika mijadala darasani na hata nje ya darasa nilifaidika sana.

Shukurani zangu za dhati nawapa wazazi wangu Marehemu babangu, Bw. Samuel Shake na Bi. Ruby Kambe kwa kunielimisha. Pia namshukuru sana mume wangu mpendwa Capt. Richard Maithya na wanangu Samuel, Yvonne na Wendy pamoja na ndugu zangu wote kwa kunipa moyo wakati nilipokuwa masomoni. Heko pia kwa jamaa na marafiki wote.

Mwisho namshukuru mpigaji chapa wa kazi hii Bi. Rina Awori.

Ahsanteni nyote

## MUHTASARI

Utafiti huu umetokana na imani kwamba ukiushi katika lugha ya kimaongezi ni tukio halisi na dhahiri katika matumizi ya lugha yo yote ile. (Taz. Max Black, 1968). Kuifahamu lugha na kuielewa kikamilifu kunahusu pia ufahamu wa hali ya ukiushi na sababu za ukiushi huo unaotokea. Tasnifu hii imechunguza na kuonyesha baadhi ya makosa (ukiushi) yanayotokea katika hali halisi ya maongezi ya wahusika kutoka katika mtaa wa Kariobangi South, mjini Nairobi.

Kazi hii imegawanywa katika sura sita. Kila sura inajadili kipengee maalum kinachohusu matumizi ya lugha. Kila sura ina utangulizi, na panapo hitajika, kiishio kinachotoa muhtasari na uamuzi wa jumla kulingana na matokeo ya utafiti.

Sura ya kwanza ni utangulizi wa utafiti. Utangulizi wa sura hii unatoa maelezo machache kuhusu mtaa wa Kariobangi South (tulikofanyia utafiti) na wakazi wake. Katika sura hii pia tumejadili somo letu la utafiti, madhumuni yetu ya kuufanya utafiti huu na upeo wa tasnifu. Zaidi ya hayo pia tumeelezea kuhusu nadharia tunayoitumia kama kigezo cha kupimia matumizi ya lugha. Katika sehemu ya 'Yaliyofanywa kuhusu somo', tunajadili baadhi ya kazi zingine zilizofanywa na kuandikwa na ambazo, kwa namna

fulani, zinahusiana na utafiti wetu. Tunatoa sababu zetu za kulichagua somo katika sura hiyo ya kwanza. Fauka ya hayo, tunatoa maelezo kuhusu haipothesia zinazopimwa katika utafiti huu na njia tulizozitumia katika kuufanya utafiti wetu.

Sura ya pili inayashughulikia masiala muhimu kuhusu lugha ya Kiswahili na matumizi yake kwa jumla. Tunaziangalia hoja za usanifishaji wa lugha na dhana ya ukiushi katika matumizi ya lugha; na kuelezea jinsi ambavyo ukiushi unadhihirika kulingana na matumizi ya lugha kimaongezi.

Sura ya tatu, ya nne, na ya tano ndizo kiini cha utafiti wetu. Tunaanza kwa kutoa hoja za kijumla kutokana na utafiti wetu. Kisha tunaiainisha data yetu na kuichanganua katika viwango vya matamshi, sarufi, na msamiati na maana. Katika kila kiwango na kwa kila kosa (ukiushi) tunatoa maelezo yanayotokana na utafiti wetu kuhusu kile kinachosababisha mzungumzaji kulifanya kosa hilo.

Sura ya sita ni hitimisho la kazi hii, ambapo tunatoa maelezo ya kijumla kuhusu utafiti wetu na matokeo yake. Pia tumetoa mapendekezo ya utafiti zaidi unaoweza kufanywa katika uwanja huu wa uchunguzi wa matumizi ya lugha ya kimaongezi.

# SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Utafiti wetu unashugulikia swala la ukiushi unaotokea katika lugha ya kimaongezi. Ukiushi katika lugha ya kimaongezi unahusu hoja mbalimbali, na kujaribu kuziainisha zote kwa pamoja na kwa ukamilifu sio jambo linalowezekana; hasa katika kazi kama hii ya tasnifu iliyowekewa mipaka ya kiwakati na iliyo na upeo maalum.

Utafiti wetu umejikita katika mambo machache kati ya nyanja zote zinazohusu matumizi ya lugha. Tunaangalia ukiushi unaojitokeza katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia, na msamiati na maana. Kazi kama hii inaweza kufanyiwa utafiti katika sehemu yo yote ile iwapo ni mijini au mashambani, mahali ambapo lugha ya kiswahili (au lugha yoyote inayofanyia utafiti) inapozungumzwa. Hii ni kwa sababu ukiushi katika lugha ya kimaongezi huweza kutokea mahali po pote kila mara lugha inapozungumzwa. Utafiti wetu tumeufanya katika mtaa wa Kariobangi South, ulioko katika sehemu za Mashariki mwa mji wa Nairobi.

Mtaa huu wa Kariobangi South una takriban nyumba elfu moja (Kulingana na hesabu yetu). Zikiwemo za aina ya 'flats' (ghorofa) zinazoishi jamii mbalimbali. Nyumba hizi zilijengwa na Halmashauri ya Jiji la Nairobi kwa minajili ya kuwapa makao wafanyikazi wa Serikali katika miaka ya

sitini na sabini. Kwa sasa ziko pia nyumba za watu binafsi walizojenga za kupangisha au kuishi wenyewe. Wengi wa wakazi wa mtaa huu ni wafanyi kazi wa Serikali na wengine wanafanya kazi katika mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile benki na biashara za kibinafsi. Hawa ni wale wanaoonekana kuwa katika tabaka la juu kiuchumi. Kuna na wale wanaofanya kazi za Jua-Kali kama vile Useremala, Uundaji magari mabovu, ushonaji viatu, na kadhalika.

Licha ya hayo, kuna shule ya msingi, shule tatu za nasari, makanisa manne (katoliki, PCEA, AIPCA na "Believers' Faith Church") na masoko mawili makubwa ya Halmashauri ya Jiji la Nairobi. Katika masoko haya mnauzwa bidhaa mbalimmbali za vyakula pamoja na nguo na viatu. Soko kuu la Kariobangi South lina pia vibanda vinavyotumiwa kwa kushonea nguo, kwa usukaji na utengenezaji wa nywele, mikahawa, na kadhalika.

Kwa hivyo tuliwateua wahusika wetu, katika kutafuta data, tukitilia maanani kwamba kwa sababu ya shughuli hizi zote zinazofanywa na wakazi wa mtaa huu ni vizuri kuwa na angalau mhusika mmoja anayewakilisha kila kundi la wafanyikazi hawa. Katika sura inayofuata, (sehemu 1.8) tumefafanua zaidi kuhusu njia za utafiti na wahusika wetu.

Mtaani Kariobangi South mnaishi watu wenye asili mbalimbali. Kwa mintarafu ya utafiti wetu, wakazi hawa wanatoka katika pande zote za nchi ya kenya. Kuna wale wanaotoka sehemu za Magharibi kama vile waluhya, Waluo, Wakisii na Wateso; kutoka sehemu za Bonde la Ufa wamo Wakalejini (km: Wanandi na Wakipisigis); kutoka katika Mkoa wa kati na wa Mashariki wamo Wakikuyu, Wameru, Waembu, Wakamba na wengineo. Wakazi wengine wametoka katika sehemu za Pwani na Kaskazini-Mashariki: nao ni kama vile Wamijikenda, Wataita na wengine wakiwa Wasomali, Waborana na Kadhalika.

Pia wakati tulipokuwa tukifanya utafiti wetu, walikuwemo wageni kutoka nchi jirani kama vile Waganda, Watanzania na Wanyarwanda.

Kiswahili ndiyo lugha inayotimika sana kama lugha ya mawasiliano kati ya wakazi hawa wa makabila mbalimbali. Baadhi yao (hasa wale waliosoma hadi kidato cha nne na zaidi) mara kwa mara hutumia lugha ya kiingereza wanapozungumza kati yao na wakati mazungumzo yao, wengine pia huchanganya ndimi (Kiingereza na Kiswahili) katika mazungumzo yao. Kuchanganya ndimi hutokea katika lugha ya wazee. Kwa mfano, mama Kamau (mhusika katika kazi yetu ya utafiti) mwenye umri wa miaka 52 mara nyingi anatumia lugha yake ya kwanza anapokuwa akifanya biashara yake ya kuuza

mboga na matunda sokoni; hata anapozungumza na mtu asiyekuwa mkikuyu. Anapogundua kwamba mteja haifahamu lugha yake ataongea "neno moja-moja" la Kiswahili kwa lugha ambayo ni "kiushi" sana ikilinganishwa na kiswahili sanifu.

Maelezo haya ni kama dibaji inayohusiana na eneo letu la utafiti. Kama tulivyokwisha taja katika muhtasari, sura hii ya utangulizi wa utafiti. Katika sura hii tumeelezea mambo kadha wa kadha yanayohitajika katika sura ya utangulizi katika vipengee mbalimbali.

## 1.1. SOMO LA UTAFITI

Tasnifu hii inahakiki swala la ukiushi katika maongezi ya kawaida dhidi ya kanuni au kaida za lugha sanifu ya kiswahili. Maongezi ya kawaida tumeyachukulia kuwa ni maongezi katika miktadha isiyo ya kirasmi na isiyo-husu mahojiano ya moja kwa moja. Data yetu inatokana na mazungumzo ya baadhi ya wakazi wa mtaa wa Kariobangi South, mjini Nairobi. Kwa hivyo tasnifu hii tumeipa mada 'Ukiushi katika lugha ya kimaongezi dhidi ya kanuni za kiswahili sanifu. Kwa mintarafu ya wanalugha;

"Hakuna ukweli kudai kwamba uongeaji wa lugha yo yote unaweza kufanywa kwa ufasaha mkamilifu; ingawa pana viwango tofauti vya ufasaha........ ukubaliano fulani katika kanuni za kimatamshi, kisintaksia na kimaana (semantiki) ni muhimu katika maongezi ya lugha". (Max Black, 1968:75).

Katika utafiti wetu tumeyashughulikia matumizi ya lugha ya kimaongezi katika viwango vya fonolojia, mofolojia, sintaksia, na msamiati na maana. Kulingana na utafiti uliofanywa (Labov, W., 1966, Milory, L., 1980 na Cheshire, J., 1982) imedhihirika kwamba matumizi ya lugha kimtindo hayawezi kuelezeka kikamilifu katika hali ya kuwa urasmi au kutokuwa na urasmi, kwa vyo vyote vile mtu anavyoweza kuelezea maana ya urasmi. Hivi ni kwa sababu kuna ukiushi mwingi wa kibinafsi kuambatana na wazungumzaji

tofauti katika miktadha mbali-mbali. Pia katika mazungumzo halisi, wazungumzaji hujaribu kulinganisha lugha yao na ya wale wanaozungumza nao. Wanaismu - jamii (Grimshaw, 1967, Homans, 1961, nk) wameielezea mbinu hii ya saikolojia ya kijamii kuwa ni kule kutaka kuvutia uwiano wa lugha inayotumika kati ya wazungumzaji ambayo kwa kiingereza wameiita, "Accommodation Model'. Ambapo mzungumzaji anataka kuiga jinsi ya uongeaji (uzungumzaji) wa mhusika mwenzake katika mazungumzo.

Kwa sababu hii tumejaribu kuelezea matumizi ya lugha katika mazungumuzo halisi kwa tahadhari sana na tukaweza kuipata data mwafaka katika kuiwasilisha kazi yetu. Mbinu tulizozitumia ili kulifikia lengo letu tumezijadili katika sehemu ya 1.8.

## 1.2 MADHUMUNI YA TASNIFU

Kama tulivyokwishataja, tunaangalia ukiushi unaojitokeza katika matumizi ya lugha ya kimaongezi. Tumekwishasema pia kwamba kujaribu kuelezea matumizi ya lugha katika maongezi halisi kama kwamba ni tukio ambalo haliwezi kubadilika ni kama kuchukuwa mtazamo wa kidhahania ambao, ingawa unapasa kutumika kwa kiwango fulani, inatubidi tujihadhari nao usitupotoshe katika uhakiki wetu.

Jenny Cheshire (1982), aligundua kutokana na utafiti wake alioufanyia huko mjini Reading, katika eneo la Berkshire nchini Uingereza) kwamba wazumgumzaji wanapokuwa katika mazungumzo ya kawaida bila kujishughulisha na urasmi wowote, ndipo wanapotumia mitindo halisia ya lugha yao na ni katika hali hiyo ambapo ukiushi wao unajitokeza kikamilifu. Kwa kutilia jambo hili maanani tumejaribu kuwaweka wahusika wetu katika hali ya 'kujisikia huru' kabisa wakati wa kuufanya utafiti wetu ili kupata data inayofaa. Jinsi tulivyolitekeleza jambo hili tumefafanua zaidi katika sehemu ya 1:8 inavyozungumzia njia zetu za utafiti.

Kwa kweli uchunguzi wa matumizi ya lugha katika muktadha ya kijamii hulenga kuainisha matumizi ya lugha katika maisha ya kila siku na wala sio "jinsi watu wanavyozungumza wakati mazungumzo yao yanapokuwa yakirekodiwa". Lakini ni kwa bahati mbaya kwamba mtafiti hawezi kuichunguza lugha bila kuirekodi data yake kwanza. Hata hivyo, kwa kutumia mbinu za utafiti tulizozitumia (Taz, sehemu 1:8.) tumeigawanya kazi yetu katika viwango vifuativyo;

(a) Matamshi (fonolojia)

(b) Sarufi (mofolojia na sintaksia)

(c) Msamiati (leksia na semantiki).

Migawanyo hii imetuwezesha kukijadili kila kipengee kwa ukamilifu wake uliostahili katika kazi hii. Hii ni sababu kwamba, katika sehemu ya fonolojia, kwa mfano, tumeyaorodhesha makosa yote ya kifonolojia yaliopatikana katika utafiti wetu na kuyajadili kulingana na miktadha yalipojitokeza na sababu inayofanya makosa kama hayo kutokea jinsi yanavyotokea. Kwa mfano, tumeona kwamba mara nyingi mtu anapojifunza lugha nyingine zaidi ya lugha yake ya kwanza, masikio na viungo vyake vya kutamkia huwa vimezeoa utaratibu fulani wa sauti (Taz. Trudgill, 1974, na Black, 1968:95), kwa hivyo tunajaribu kuonyesha jinsi,

(a) Upungufu katika lugha ya kwanza wa vitamkwa (fonimu) ambavyo vinapatikana katika lugha ya kiswahili, unavyoweza kuathiri matumizi ya lugha katika maongezi. Pia jinsi fonimu zinazopatikana katika utafiti wetu.

(b) Matumizi au mipangilio tofauti ya kisarufi inavyotatanisha matumizi ya lugha iwapo miundo hiyo inatofautiana kati ya lugha ya kiswahili na lugha ya kwanza ya mzungumzaji, au kutokana na sababu zo zote zile tutakazozipata katika utafiti wetu.

(c) Tofauti za kimsamiati na/au kisemantiki zinazotokana na tofauti za kiutamaduni katika lugha ya kwanza ya mzungumzaji na kiswahili.

Kwa kufanya haya tunalenga hasa kufanya mambo mawili muhimu yanayohusu utafiti huu.:-

(1) Kuorodhesha aina zote za makosa (ukiushi) yanayojitokeza katika mazungumzo ya wahusika dhidi ya kanuni za lugha ya kiswahili sanifu.

(2) Kujaribu kutoa maelezo mwafaka, yanayotokana na uchunguzi wetu, ya mambo yanayosababisha ukiushi au makosa wanayoyafanya wazungumzaji.

## 1.3 UPEO WA TASNIFU

Ukiushi katika lugha ya kimaongezi unahusu hoja mbalimbali na kujaribu kuziainisha zote kwa pamoja si jambo linalowezekana hasa ikiwa mtu anataka kulifanya jambo hili kwa njia ya ukamilifu. Pia katika kazi ambayo imebanwa kwenye mipaka ya kiwakati na iliyopewa upeo maalum sharti mtafiti achague mwelekeo fulani na vipengee fulani vya kufanyiwa utafiti.

Utafiti wetu unashughulikia swala la ukiushi unaotokea katika lugha ya kimaongezi. Na kama tulivyokwisha kugusia katika sehemu ya 1:1, utafiti huu unashughulikia hasa maongezi ya kawaida ambayo tumeyaelezea kama maongezi yasiyokuwa katika miktadha ya kirasmi.

Uhusiano kati ya hali za kiuchumi na uzungumzaji wa lugha "kiushi" (au pijini) kati ya waongeaji ni jambo ambalo limewahi kujadiliwa sana na wanaismu-jamii (Taz. Milroy, L., 1980; Macaulay, R.K.S., 1977; Labov W., 1968; nk). Katika tasnifu hii hatujakusudia kujishughulisha na utafiti wa hali za kiuchumi za wahuskika wetu. Kama tulivyokwishakutaja kazi yetu inashughulika tu ukiushi unaotokea katika hali halisi ya kimazungumzo bila kutilia maanani hali za kiuchumi za wahusika. Data yetu tumeichanganua katika viwango vitatu muhimu.

(a) Matamshi (fonolojia).

(b) Sarufi (mofolojia na sintaksia)

(c) Msamiati (leksia na semantiki).

Mtafiti ye yote anayetaka kufanya kazi ya kiwango cha juu sharti ateue nyanja fulani za kushughulikia kuliko kujadili mambo mengi kwa pamoja. Kwa mfano kuna mengi ya kutafitiwa na kujadiliwa kuhusu matumizi ya lugha, lakini tumeziteua sehemu hizi tatu ili tuweze kuzishughulikia kikamilifu.

## 1.4 SABABU ZA KULICHAGUA SOMO

Kiswahili, kama lugha ya Taifa la Kenya, kilitambuliwa rasmi katika mwezi wa Agosti, mwaka wa 1969 (Taz. Chiraghdin, S., Mnyampala, M, 1977:80). Kwa hivi sasa

kiswahili ni mojawapo ya masomo muhimu yanayotahiniwa katika viwango vyote vya elimu katika mitihani ya kitaifa. Lugha ya kiswahili pia ndiyo inayoyaunganisha makabila yote ya nchi ya Kenya (hata pia nchi nyingine jirani) katika mawasiliano.

Hivyo basi tunapaswa kuwa na lugha thabiti ya kiswahili ambayo itatumika kama chombo mwafaka cha kuyafikia na kuyatimiza matamanio na malengo yetu katika maendeleo ya nchi hii.

Katika maingiliano baina ya watu hapana budi kuwe na kuathiriana. Katika kuathiriana huku lugha ya Kiswahili imeibuka na "vilugha" (pijini) vinavyozungumzwa katika sehemu mbalimbali. Kwa sababu ya umuhimu wa lugha hii hapa nchini Kenya (kama lugha ya taifa inayowaunganisha WaKenya) hatuna budi kuhakikisha kwamba tunaimudu lugha hii kikamilifu na kwamba tunajitahidi katika kuindeleza kwa manufaa ya nchi yetu.

Utafiti kama huu umefanywa kuhusu lugha nyingi za ulimwengu, hasa lugha ya kiingereza (Taz. sehemu ya 1:6 'Yaliyofanywa kuhusu somo'), Tunavyofahamu sisi, kulingana na utafiti wetu, ni kwamba kufikia leo hakuna uhakiki wo wote uliofanywa, ukitumia nadharia za kiuhakiki, katika matumizi ya lugha ya kiswahili kimaongezi katika hali

halisi ya maongezi ya wahusika. Kazi zilizofanywa (Taz. Mbaabu, I, 1978 na Gilman, C., 1976) ni kazi zilizofanywa bila kufuata misingi ya nadharia ya lugha wala hazikufanyiwa utafiti unaohusu eneo fulani bali ni uainishaji wa makosa yanayokisiwa kuwa hufanywa na wazungumzaji. Kazi nyingine pia ambayo ilihusu matumizi ya lugha ni tasnifu ya Nyauncho, O.K. (1985) ambayo iliangalia matumizi ya "kisheng" na sio katika muktadha wa kiilinganisha na lugha sanifu ya kiswahili. Imeangalia jinsi lugha hii ilvyoibuka na ni akina nani wanaoitumia.

Tunatarajia kwamba kazi hii itakuwa kielelezo bora cha kufanywa utafiti zaidi wa lugha hii ya kiswahili ili wapangaji wa sera za lugha wapate mwelekeo bora na kujitahidi zaidi katika kuiendeleza.

## 1.5 <u>HAIPOTHESIA</u>

Utafiti wetu unatathmini haipothesia zifuatazo;

(a) Makosa mengi yanayofanyika ni makosa ya kimatamshi, na kwamba yanatokana na athari za lugha za kwanza za wazungumzaji.

(b) Makosa yanayojitokeza zaidi katika mazungumzo ya wakazi wa mtaa wa Kariobangi South ni makosa ya kisintaksia na kileksia.

(c) Ukiushi katika matumizi ya lugha unatokana na mazingira. Kwamba, hata mzungumzaji ambaye, kwa mfano, lugha yake ya kwanza ni Kikisii atatumia matamshi na miundo ya lugha na msamiati wa lugha nyingine (km kikuyu) katika maongezi yake kwa sababu ya kutangamana na kuishi nao katika mazingara mamoja.

## 1.6 YALIOANDIKWA KUHUSU SOMO HILI

Kazi nyingi zimewahi kufanywa kuhusu swala la ukiushi katika matumizi ya lugha ya kimaongezi. Jenny Chesire (1982) alifanya utafiti wake huko mjini Reading, Berkshire, nchini Uingereza. Utafiti wake ulihusu ukiushi katika miundo ya kimofolojia na sintaksia kati ya wahusika 24 wakiwa ni wasichana na wavulana wa umri kati ya miaka 9 na 17 (tisa na kumi na saba). Matokeo yake ni kwamba wahusika walifanya makosa mengi zaidi walipokuwa nje ya shule kuliko yale waliyofanya walipokuwa katika mazingira ya shule. Pia aligundua kwamba mahali mtu anakotoka humwathiri katika matumizi yake ya lugha kutokana na uzungumzaji aliojizoeza.

J.J. Gumperz (1971) akishirikiana na C.M. Naim walifanya utafiti wao kuhusu ukiushi dhidi ya lugha au lahaja sanifu ya kihindi. Wamezungumzia juu ya tofauti za kiismu zinazotokana na mazingira ya kijamii na uhusiano kati ya lahaja kiushi na jamii ya mzungumzaji.

Kwa upande wa lugha ya kiswahili, K.O. Nyaucho (1985) katika tasnifu yake ya B.A. ameshughulikia "Kisheng" ambayo ni 'lugha' chipuko dhidi ya lugha ya kiswahili. Ameonyesha tofauti za miundo ya lugha na msamiati unaopatikana katika "kisheng" na kuonyesha kwamba hii ni lugha inayozungumzwa sana na watoto (hasa katika sehemu za mashariki mwa jiji la Nairobi) kuliko na watu wazima.

Naye I, Mbaabu (1978:45 - 89) ameyaainisha makosa yanayotokana na maingiliano kati ya lugha za kwanza na maongezi ya kiswahili. Ameshugulikia takriban lugha kumi za WaKenya na kuonyesha jinsi zinavyoweza kuyaathiri matumizi ya lugha ya kiswahili kati ya wazungumzaji.

Kwa kweli swala la lugha na matumizi ya lugha limekuwa muhimu kati ya wanaismu, wanaismu - jamii na hata pia wale wanaoshughulikia lugha katika kiwango cha kisaikolojia. (Taz. Grimshaw, 1967 ha Homans, 1961). Hata Labov, (1966) alilishughulikia swala la ukiushi wa lugha ya kimaongezi huko "Lower East Side", New York, ambapo alitumia miktadha ya mazungumzo ya kirafiki katika kuitafuta data yake.

## 1.7 MISINGI YA NADHARIA

Nadharia tutakazozitumia katika kuangalia matumizi ya lugha katika maongezi ni nadharia za kiuhakiki. Kwanza tutaiegemea nadharia ya umuundo ambayo inaainisha lugha

kulingana na miundo yake ya kisarufi. Ni katika nadharia hii ambapo tunapata kigezo cha kuweza kuainisha kati ya lugha sanifu na ukiushi dhidi ya kanuni za hiyo lugha sanifu ya kiswahili (kama tunavyozifahamu kutokana na utafiti wetu wa maktabani wa kuvipitia vitabu vya sarufi na makamusi ya kiswahili sanifu).

Kwa kawaida matumizi ya lugha sharti yafuate sheria au kanuni za kisarufi; lakini pia matumizi haya hutegemea uteuzi wa mzungumzaji. Kwa minajili ya F. de Saussure (1961) 'langue ni ule uwezo wote wa kuitumia lugha fulani ambao mtu anaupata kutoka kwa jamii yake wanaozungumza lugha hiyo. 'Langue' inaweza pia kufafanuliwa kuwa ni sheria zote za kisarufi kuhusu lugha ambazo jamii inayozungumza lugha hiyo inazitambua. Kwamba mtu anaifahamu lugha na kuzijua sheria zake, si kwamba lugha hiyo ataitumia kwa ufasaha mkamilifu. Katika hali halisi ya mazungumuzo, 'parole', mzungumzaji atautumia uwezo alio nao wa lugha hiyo kulingana na uteuzi wake.

Kwa kutilia dhana hizi za 'langue' na 'parole' maanani, tumechukua mwelekeo huu wa F.de Saussure unaobainisha kati ya 'langue' na 'parole' ili kuweza kutathminia ukiushi unaojitokeza katika hali halisi ya maongezi ya wahusika wetu wa mtaa wa Kariobangi South.

Geoffrey Leech (1969) anatazama matumizi ya lugha kimtindo katika viwango hivi;

(1) Kiwango cha utendaji.

(2) Kiwango cha umbo.

(3) Kiwango cha semantiki.

Kiwango cha utendaji kinahusu vile lugha inavyotamkwa na kuandikwa (fonolojia na grafolojia). Kwa minajili ya kazi yetu ambayo inshugulikia lugha kimaongezi kiwango hiki ni cha fonolojia. Katika kiwango hiki tungetaka pia kuangalia kiimbo na mkazo (msistizo) lakini haiwezekani kwa sababu ya ukubwa wa kazi yetu na uchache wa muda wa kuishughulikia. Kwa hivyo tunaangalia mabadiliko ya sauti katika maongezi ya wahusika na matamshi yao ikiwa yamekiuka kanuni za lugha sanifu ya kiswahili.

Kiwango cha umbo kinahusisha msamiati uliotumika kujenga sentensi kwa mambo ya sarufi na leksia (msamiati). Kulingana na kazi yetu, tunaangalia maneno na miundo ya sentensi zilizovunja kaida za lugha kimofolojia na kisintaksia. Tunaangalia pia maneno na sentensi hizi katika kiwango cha semantiki. Katika sehemu ya leksia tunachunguza matumizi ya msamiati. Tunaangalia maneno yanayoingizwa katika msamiati wa kiswahili ambayo si ya kiswahili sanifu. Tunaweza kupata maneno yanayoingizwa kutoka kwa lugha za kwanza za wazungumzaji, na jinsi maneno

haya yanavyoiathiri lugha ya kiswahili kisintaksia na kisemantiki.

Katika kiwango cha semantiki tunaangilia jinsi matumizi ya lugha yanvyoathiri maana kwa njia fulani. Kwa mfano uteuzi wa msamiati fulani huenda usilete maana iliyokusudiwa katika sentensi fulani.

Viwango vingine ambavyo amevitaja Leech (1969) kwa kuviita matawi ya ismu ni elimu - lahaja ambayo huangalia tofauti za lugha kulingana na mtumiaji, sajili inayojihusisha na tofauti za lugha kulingana na kazi yake.

Hii ndiyo mitazamo tuliyoona kwamba inafaa kwa kazi yetu.

## 1.8 NJIA ZA UTAFITI

Katika kuishughulikia kazi hii inayohusu matumizi ya lugha, utafiti wetu umeanzia maktabani ambapo tumeweza kujiandaa kinadharia kabla ya kuingilia utafiti wenyewe uwanjani. Licha ya kuyaangalia maswala ya nadharia maktabani imetubidi pia tuvitalii vitabu vinavyozungumzia juu ya sarufi ya lugha ya kiswahili sanifu ili pamoja na ujuzi wetu wa kibinafsi wa lugha hii tuweze kutathminia na kubainisha ukiushi katika maongezi ya wahusika wetu.

Wahusika tuliowatumia katika utafiti wetu ni jumla ya watu 34 (thelathini na nne). Hawa wakiwemo wake kwa waume wenye umri baina ya miaka 18 na 60. Sababu mojawapo ya kuwateua wahusikana wa umri hizi ni kwamba hatukutaka kukumbana na matumizi ya 'kisheng' ambayo yamedaiwa (Nyancho, O.K., 1985, tasnifu ya B.A) kuwa ni lugha inayotumiwa na vijana. Kwa hivyo tumechukulia kwamba mtu anapofikia umri wa miaka 18 anakuwa amemaliza shule ya sekondari na anachukuliwa na jamii yake kuwa kama mtu mzima. Kwamba anatarajiwa na jamii yake kuchukua nafasi yake katika harakati za kuyaendeleza maisha ya jamii yake. Kwa sababu tumeona kwamba wanapotumia 'sheng' ni wakati wanapozungumza na watu wa makamo yao (ambapo pia ni kwa kiwango kidogo) au wanapozungumza na wadogo zao kiumri. Kati ya hawa wahusika wetu wamo wake 15 na waume 19. Wote pamoja ni jumla ya wahusika 34. Tumechukuwa idadi hii ya watu kuwasilisha wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili mtaani Kariobangi South kwa sababu tumeona kwamba tunaweza kushughulikia watu wachache kwa ukamilifu zaidi kuliko watu wengi. Idadi hii imetuwezesha kufanya utafiti wa maongezi yao katika miktadha na sajili mbalimbali ambayo imetupatia data mwafaka katika kazi hii.

Jambo lingine muhimu tulilolizingatia ni aina ya wahusika. Licha ya kwamba tumeteua wanawake kwa waume tumejaribu kuhakikisha kwamba hawa wanafanya shughuli

mbalimbali katika maisha yao ya kila siku. Hili linatupatia upeo mkubwa wa kuyatathmini matumizi ya lugha katika miktadha na sajili mbalimbali ili tuweze kulifikia lengo letu (Taz. sehemu 1.2) kikamilifu. Kijalizo kilichoko hapa chini kinaelezea zaidi kuhusu wahusika wetu.

## KIJALIZO

### SOKONI

| | JINA | UMRI | MKE/MUME | KAZI AIFANYAYO | KABILA | KIWANGO CHA ELIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Bi. Njuguna | 39 | mke | Mshona Nguo | Mkikuyu | Kidato cha 4 |
| 2. | Bw. Onyango | 32 | mume | mshona nguo | Mjaluo | Darasa la 7 |
| 3. | Mama Wambua | 32 | mke | muuza mboga na matunda | Mkamba | (haijulikani) |
| 4. | Mama Kamau | 52 | mke | muuza mboga na matunda | Mkikuyu | Hajasoma |
| 5. | Mary | 28 | mke | Msusi | Mluhya | kidato cha 4 |
| 6. | Njeri | 19 | mke | Msusi | Mkikuyu | kidato cha 2 |
| 7. | Baba Mwangi | 45 | mume | muuza nyama | Mkikuyu | (haijulikani) |
| 8. | Muturi | 39 | mume | muuza nyama | Mweru | Darasa la 7 |

### KANISANI

| | JINA | UMRI | MKE/MUME | KAZI AIFANYAYO | KABILA | KIWANGO CHA ELIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9. | Jeremiah | 56 | Mume | Mzee wa kanisa | Muembu | (haijulikani) |
| 10. | Mama Roda | 41 | mke | mwenye kiti wa "Mothers Union" | Mkikuyu | (Haijulikani) |
| 11. | Beatrice | 36 | mke | Mama wa kanisa | Mkikuyu | Kidato cha 4 |
| 12. | Peter | 49 | mume | muuza duka | Mkikuyu | (haijulikani) |
| 13. | Mama Jane | 36 | mke | muuza duka | Mteso | kidato cha 4 |
| 14. | Oduori | 19 | mume | msaidizi wa mama Jane | Mluo | darasa la 8 |

### MADUKANI

| | JINA | UMRI | MKE/MUME | KAZI AIFANYAYO | KABILA | KIWANGO CHA ELIMU |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 15. | "Customer" | 34 | Mume | Muuzaji mahindi-choma | Mkikuyu | (haijulikani) |
| 16. | Mwangi | 21 | mume | muchuuzi wa peremende na sigara | Mkikuyu | Darasa la 7 |
| 17. | Oloo | 57 | mume | Mshona viatu | Mjaluo | - |
| 18. | Bw. Maranya | 58 | mume | mfanyi biashara | Mkisii | kidato cha 4 |
| 19. | Bi. Maranya | 43 | mke | mwalimu wa shule ya msingi | Mtaita | kidato cha 6 |
| 20. | Bw. Nzioka | 38 | mume | afisa wa serikali | Mkamba | Kidato cha 4 |
| 21. | Bi Nzioka | 31 | mke | hajaajiriwa | | |
| 22. | Bw. Kipkoriri | 43 | mume | Meneja wa kampuni | Mnandi | shahada ya B.A |

| JINA | UMRI | MKE/MUME | KAZI AIFANYAYO | KABILA | KIWANGO CHA ELIMU |
|---|---|---|---|---|---|
| 23. Bi. Kipkorir | 38 | mke | mwalimu wa shule ya upili | Mnandi | Diploma ya walimu |
| 24. Bw. Obiero | 52 | mume | menja wa Benki | mjaluo | Shahada ya B.A. |
| 25. Bi. Obiero | 48 | Mke | Anafanya kazi ya kuuza nguo. | Mjaluo | Kidato cha 4 |
| 26. Akinyi (binti ya Obiero) | 18 | mke | Anafanya kazi ya usekretari. | " | kidato cha 4 |
| 27. Mama Shem | 31 | mke | mwalimu wa shule ya msingi | Mjaluo Mbukusu | kidato cha 4 chuo cha ualimu |

WAFANYI KAZI JUA - KALI

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 28. Kariuki | 28 | mume | mtengenezaji wa magari mabovu | mkikuyu | Kidato cha 4 |
| 29. Odhiambo | 34 | mume | " " | mjaluo | Darasa la 7 |
| 30. Ibrahim | 46 | mume | Seremala | " | hajasoma |
| 31. Lukalo | 25 | mume | " " | mluya | Darasa la 7 |

WENGINEO

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 32. Mzee Hassan | 58 | mume | mlinzi wa nyumba | Mborana | hajasoma |
| 33. Anna | 20 | mke | Mfanyikazi nyumbani | muembu. | darasa la 5 |
| 34. Kimeu | 29 | mume | mlinzi wa usiku | mkamba | darasa la 7 |

Tunaweza pia kuwasilisha idadi ya wahusika kulingana na umri katika migawanyo minne ya kati ya miaka kumi katika kundi.

| Umri (miaka) | Idadi ya wahusika |
|---|---|
| 18 - 28 | 8 |
| 29 - 39 | 14 |
| 40 - 50 | 6 |
| 51 - 60 | 6 |
| | 34 (Jumla) |

Pia tumeangalia viwango vyao vya elimu kuweza kubainisha ikiwa elimu inaweza kuathiri matumizi ya lugha ya kiswahili. Kwa mfano ikiwa elimu imewathiri mzungumzaji kwa kuzungumza kwa ufasaha zaidi au ikiwa kiwango cha elimu hakitofautishi matumizi ya lugha kimaongezi. Pia ikiwa elimu imewafanya wapendelee kutumia maneno ya Kiingereza katika Kiswahili na miundo ya lugha ya Kiingereza katika sentensi za Kiswahili.

Sababu ya kuchagua wanaume na wanawake ni kwamba tunataka kuchunguza aina zote za ukiushi katika mazungumzo ya wakazi wa mtaa huu wa Kariobangi South kwa jumla, kwa hivyo tunapata ukiushi fulani ambao labda haukujitokeza katika mazugumnzo ya wanaume. Kwa mfano, katika upande wa msamiati wa sokoni mama Wambua na mama Kamau walipendelea

kutumia sana majina ya lugha ya Kikuyu (kama vile "mbosho" "dhooko" na "rufia," ambayo ni maharagwe, kunde, na shilingi mbili kwa lugha ya kiswahili).

Katika utafiti wetu ilitubidi kutumia mbinu ya mshiriki - mtafiti ili kupata mazungumzo halisi yanayohusu ukiushi wa kimaogezi. Kulingana na "Accomodation Model" kama ilivyoelezewa na Grimshaw (1967) wahusika wanapotambua kwamba mazungumzo yao yanarekodiwa au wanapohojiwa watajaribu kuyaboresha au mara nyingi hujaribu kuilinganisha lugha yao na ya yule anayewahoji. Jambo hili halitoweza kutoa data halisi ya ukiushi wao wa kawaida katika mazungumzo ya kila siku. Kwa hivyo mbinu tuliyoitumia, na ambayo ilifaa sana, ni ile ya kukibeba kinasa sauti ndani ya mkoba au kikapu, kama mzigo, wakati tulipotaka kurekodi data kutoka kwa wahusika wetu. Mara mazungumzo yalipoanza tuliingiza mkono mkobani, ambao tulihakikisha kuwa uko wazi, na kufungulia kinasa-sauti. Hili halikuwa jambo gumu kwetu sisi na njia hii ilitusaidia sana kupata data ambayo ilioana na lengo letu (kupata ukiushi wa kimaongezi kama unavyojitokeza katika mazungumzo ya kawaida).

Katika vipindi vya kurekodia sokoni, ilitubidi kwenda wakati wa mchana (kuanzia saa nne hadi saa tisa) wakati ambapo hakuna wateja wengi sokoni. Soko hili ni soko la

'kisasa' lililo na vibanda viliyopangwa sawasawa kwa hivyo mara nyingi hapana msongamano na makelele yanayotokea katika masoko mengine yasiyojengwa kwa utaratibu bora. Tulitumia mbinu hii ya kurekodi katika kanda za kinasa - sauti.

Mbinu nyingine tuliyoitumia na ambayo ilitufaa katika kufanyia utafiti kanisani ni ile ya kunakili sentensi zenye ukiushi. Tulizinakili sentensi hizi moja kwa moja kwenye karatasi kama tulivyozisikia. Hili halikuwa jambo gumu kwa sababu mara kwa mara watu hunakili vifungu vya Biblia na matangazo muhimu wanapokuwa kanisani. Ni wakati wa matangazo ya kila Jumapili kanisani ambapo tulipata data ya ukiushi kutoka kwa Jeremiah, mama Rodah, na Beatrice.

Baada ya kurekodi na kunakili data yetu tulikaa chini na kuanza kuyaorodhesha na kuyaainisha makosa yote tuliyoyapata. Makosa mengi, hasa yale ya kimatamshi yalikuwa yamerudiwarudiwa mara nyingi katika miktadha mabalimbali. Ilitubidi kuyachanganua kulingana na miktadha na kuteua miktadha itakayotosheleza katika kuyawasilisha matokeo ya utafiti wetu. Makosa haya yote yamechunguzwa kulingana na nadharia zetu na kwa minajili ya madhumuni yetu. Tunayachambua na kuyahakiki na tunadokeza sababu zilizofanya makosa haya kutokea kulingana na utafiti wetu kati ya wahusika wetu. Mbinu nyingine tuliyoitumia katika uhakiki wetu ni kama wanavyosema Halle na Stevens (1964);

"....anayeisikia lugha yo yote (ikizungumzwa), ikiwa anaifahamu lugha hiyo, atazitambua arki za kifonolojia pamoja na (arki) za kimsamiati na kisarufi katika usemi fulani kwa njia inayojulikana kama 'uchanganuzi kwa uunganishaji." (Tafsiri yetu).

Hivi ni kusema kwamba, katika utafiti wetu na uchanganuzi wa data pia tumetumia ujuzi wetu wa lugha ya kiswahili.

## 1.9 HITIMISHO

Kulingana na maelezo haya, ambayo kama tulivyokwisha kusema ni kama utangulizi wa kazi yetu kwa jumla, tumeonyesha mambo muhimu ambayo yametuelekeza na kutuandaa katika kuziainisha sura zifuatazo. Tumekwisha kuelezea mada yetu na nadharia zetu, au mitazamo tuliyoichukua katika kutafiti na kuianisha data yetu na kulingana na hayo yote tukalifikia lengo letu (au malengo yetu hasa) kama tulivyojadili katika kipengee cha 1.2 katika sura hii ya utangulizi.

Kwa kuihitimisha sura hii tungependa kutaja kwamba hatukuweza kupata data ya kutosha kutokana na wahusika wetu. Kama inavyodhihirika katika sura ya tatu, ya nne, na ya tano, tumepata data nyingi zaidi kutoka kwa wahusika fulani kuliko kwa wahusika wengine. Hivi ni kwa sababu

hatukuweza kupata vikao vya kutosha ili kupata data kubwa kutoka kwa wahusika kama vile Bw. Kipkorir, Bi. Kipkorir, Bw. Obiero, Bw. Nzioka, Kariuki, na Lukalo ambao mara nyingi hawakupendelea kujihusisha katika mazungumzo. Hata hivyo, data tuliyoipata kwa jumla imetosheleza katika kuiwasilisha kazi yetu.

## SURA YA PILI

## 2.0 LUGHA NA MATUMIZI YAKE KATIKA JAMII

### 2.1 UTANGULIZI

Katika kuangalia ukiushi unaotokana na matumizi ya lugha katika jamii, ni muhimu kwanza tujaribu kuifafanua kwa kifupi dhana hii ya lugha. Dhana ya lugha hi hoja ambayo imewahi kujadiliwa na kufafanuliwa na wanalugha kwa namna mbali mbali. Tunapojaribu kuijadili sharti ikumbukwe kwamba lugha ni dhana telezi mno. Katika kila maelezo yanayotolewa panaweza pia kupatikana ufafanuzi badalia wa kuwasilishia jambo hilo hilo. Hivi ni kusema kwamba, tunaweza kutoa maelezo kwa njia mbali mbali katika kuifafanua dhana ya lugha.

Katika juhudi zao za kuifafanua hoja hii, wanaismu (km: Sapir, 1921) wamejitokeza na maelezo kwamba lugha ni:-

> "njia ya kuwasilishia mawazo, hisia na matamanio kwa matumizi ya utaratibu wa ishara zinazotoka huru miongoni mwa binadamu"[1] (tafsiri yetu)

Kimsingi ishara hizi hujitokeza kama sauti ambazo hutokana na vifaa vinavyojulikana kama viungo (ala) vya matamshi ambavyo mtu huzaliwa navyo ingawa hazaliwi na ujuzi wa lugha.

Lugha pia imefafanuliwa kama,

> "utaratibu wa taashira za sauti zinazotoka huru pamoja na ishara za kisarufi ambapo jamii ya waongeaji inaweza kuwasiliana na kupokezana utamaduni wao".[2]
>
> (Tafsiri yetu.)

Aidha swala la lugha ni pana mno. Maelezo haya machache yanatuangazia juu ya kile kinachoitwa lugha ili kutuwezesha kuihimili kazi yetu inayoshunghulikia matumizi ya lugha kimaongezi.

Katika sehemu hii tunalizungumzia swala hili la lugha na matumizi yake tukizingatia matumizi ya lugha kwa jumla, hali ya lugha nchini Kenya, hoja ya lugha sanifu, dhana ya ukiushi, na hali ya lugha mjini Nairobi.

## 2.2 MASIALA MACHACHE KUHUSU MATUMIZI YA LUGHA

Licha ya kuwa lugha ndicho chombo cha mawasiliano baina ya watu wa jamii fulani, lugha pia,

"ndiyo msingi wa maingiliano kati ya watu na ndicho kitu kikuu kinachowaunganisha watu katika makundi. Huwapa wanadamu utambulisho wa hali ya kujihisi kwamba wao ni watu wa kushirikiana katika kufanya kazi pamoja kwa manyaa ya wote."[3]

(Tafsiri yetu)

Kwa mujibu wa haipothesia iliyopendekezwa na Sapir na Whorf[4] ambayo pia hujulikana kama haipothesia ya Whorf' (Whorfian hypothesis),

"Lugha anayoizungumza mtu kama lugha yake ya kwanza hukuza aina za kategoria ambazo huwa kama kigezo cha kupimia jinsi anavyouhisi ulimwengu wake au jinsi anavyozipanga na kuzielewa dhana mbalimbali. Lugha huweza kuathiri jamii fulani au hata pia kuuongoza mtazamo kuhusu maisha wa waongeaji wake." (Tafsiri yetu).

Uhusiano baina ya lugha na wazungumzaji ni kwamba hautenganishiki. Kila neno analoliongea mtu huwa ni kifaa cha kumfunza kuhusu mazingira yake na jinsi binadamu anavyoyakabili katika harakati zake za kujiendeleza katika maisha. Kwa kutilia maanani kwamba lugha ndicho chombo kibebacho utamadumi wa mzungumzaji, A. A. Mazrui, (1975:185) anasema kuwa ni jambo lisilo la kawaida kutenganisha lugha

na utamaduni maana mtu hawezi kujifunza vyema kuhusu utamaduni wa Wafaransa kwa kutumia kihindi au kiarabu. Ili mtu kuupata utamaduni wote wa Wafaransa, kwa mfano, lazima utamaduni huo umfikie kwa lugha ya kifaransa maana fikira za watu na lugha wanayoiongea ni mambo yaliyofungamana.

Kutokana na hali hii, tunaweza pia kusema kuwa lugha hutumiwa ili kuleta umoja katika jamii fulani. Katika kuifanya jamii kuweza kujitambulisha, inaiunganisha na kuifanya ijihisi kama jamii inayothamini mambo mamoja na jinsi ya kuendeleza maisha. Lugha hufungua na wakati huo huo ikasisimuwa hisia za muungano wa kikabila au kitaifa pale inapojitokeza na kujidhirisha kama chombo cha umoja miongoni mwa wazumgumzaji wake.

Lugha ni tukio la kijamii. Katika jamii yenye kuongea lugha tofauti tofauti na yenye tamaduni mbalimbali hutokea hali ya kuathiriana kwingi. Athari hizi hutokea katika viwango tofauti tofauti. Kwa mfano katika hali ya 'lugha katika mgusano' hutokea 'ukopaji' na 'ukopeshaji' wa msamiati na pengine pia hutokea mabadiliko ya kisauti. Ni katika hali kama hii ambapo wazungumzaji wa lugha ya kiswahili huenda wakadhihirisha athari za lugha zao za kwanza. Ndipo tumewahi kupata misemo ya kwamba mtu 'anaongea kiswahili cha kiluhya' au mtu 'anaongea kiswahili kama Mkikuyu' na kadhalika."

Mahali lugha yo yote inapotumiwa na watu wengi, huibuka matumizi ya lugha kwa namna tofauti tofauti ambapo tunapata lugha za 'kimtaa'. Lugha hizi yamkini huwa na ukiushi mwingi dhidi ya lugha sanifu. Halliday (1980:81) amesema kwamba,

> "Lugha ni chombo cha kuelezea na kuuhimili muundo wa jamii fulani .....mara nyingi katika maisha halisi tunapata daraja za kilahaja na miundo tofauti ambapo lugha sanifu inakinzana na matumizi yasiyosanifika."
>
> (Tafsiri yetu).

Ni katika kuzizingatia hoja hizi ambapo utafiti wetu umenuia kuonyesha matumizi ya lugha katika miktadha ya maongezi ya kawaida (ya kila siku) ya Wahusika kutoka mtaa wa Kariobangi South, mjini Nairobi.

## 2.3. HALI YA LUGHA NCHINI KENYA (Muhtasari).

Kuna takriban lugha arobaini zinazozungumzwa nchini Kenya.[5] Idadi hii haiwezi ikakatiwa kauli kwa yakini kwa sababu baadhi ya lugha hizo huenda, wakati mwingine, zikahesabiwa kuwa ni lahaja za lugha moja. Kwa mfano ikiwa lahaja 'X' na lahaja 'Y' zinafanana (kuwa waongeaji wa 'X' na wa 'Y' huelewana) kisha 'Y' ikafanana na 'Z', ikiwa lahaja 'X' na Z hazifanani basi itakuwa vigumu kuzitambua

ikiwa ni lugha tofauti au lahaja tofauti za lugha moja.

Baadhi ya lugha zenye lahaja tofauti tofauti hukanganya kwa namna hii. Kwa mfano lahaja za kiluhya (kama vile Kimaragoli, Kibukusu, Kiidakho, Kikabras na kadhalika) mara nyingine baadhi ya lahaja hizo huhesabiwa kama lugha tofauti badala ya lahaja za lugha moja (km.Kimaragoli). Pia limekuwa swali la mjadala ikiwa Kitharaka ni lahaja ya Kimeru, ya Kikuyu au ni lugha ya pekee isiyo lahaja ya lugha nyingine.

Hata hivyo, makundi muhimu ya lugha yanayojitokeza ya Wakenya Kindakindaki ni kama vile Wabantu, Wanailoti, na Wasemiti. Kuna pia lugha zilizoletwa na wageni kwa vile kiarabu, kihindi, kiingereza na kigujarati. Waaidha kuna mseto wa lugha nchini Kenya.

Kwa kifupi hali ya lugha nchini Kenya yaweza kugawanywa katika sehemu tatu. Kwanza ni lugha za kwanza au lugha za mama. Lugha hizi ni kama vile Kikamba, Kidholuo, Kikalenjin, Kisamburu, na Kirendille. Lugha za kwanza ndizo zinazotumika sana kwa jumla ingawaje kila moja-wapo hutumiwa na idadi ndogo ya Wakenya.

Sehemu ya pili ni lugha ya Kiswahili. Kiswahili hutumiwa na watu wachache sana kama lugha ya mama. Wengi

wa wale wanao-kitumia kiswahili wana lugha nyingine kama lugha zao za kwanza. Kwa hivyo kiswahili kina jukumu kubwa katika kuwaunganisha wananchi kutoka jamii na asili mbali-mbali.

Kiingereza kinachukuwa sehemu ya tatu. Hivo ndiyo lugha inayotumiwa katika elimu ya juu, sheria na biashara kubwa kubwa kama vile utalii, bima na mabenki. Kiingereza pia chatumika sana katika mawasiliano kati ya Kenya na nchi mbalimbali za ulimwengu. Kutokana na utalii na mikutano ya kimataifa nchini Kenya lugha nyingine muhimu zinazojitokeza ni kama vile Kifaransa na kijerumani.

Uhusiano kati ya matumizi ya kiingereza na kiswahili ni kwamba kiingereza ndiyo lugha rasmi kwa shughuli nyingi za kiserikali. Kiswahili ni lugha ya taifa ambayo pia imetambuliwa kama lugha ya majadiliano bungeni. Kiswahili na kiingereza hutumika katika vyombo vya mawasiliano kama vile radio, televisheni na magazetini. Katika redio na televisheni lugha ya kiswahili hutumika kwa masaa mengi zaidi kuliko kiingereza. Hata hivyo katika stesheni ya televisheni ya 'Kenya Television Network' (KTN) ni kiingereza pekee kinachotumika. Labda hii inatokana na sababu kwamba kituo hiki ni chipuko la kituo kikuu cha kimataifa cha Marekani kinachoitwa 'Cable News Network' (CNN) ambacho hutumia lugha ya kiingereza.

Kwa upande wa magazeti, nakala nyingi zaidi hutolewa kwa magazeti ya kiingereza kuliko yale ya kiswahili. Pia magazeti ya kiingereza huchapisha habari nyingi zaidi kuliko yale ya kiswahili. Mambo haya yanaweza kuelezeka tukizingatia kwamba masomo shuleni yanafunzwa kwa lugha ya kiingereza (isipokuwa tu somo la lugha ya kiswahili na fasihi yake). Kutokana na hayo watu huzoea kusoma kiingereza kuliko kiswahili. Baada ya muhtasari huu unaotaja kwa kifupi hali ya lugha nchini Kenya kwa jumla, hebu sasa tuangalie pia jinsi hali ya lugha ya kiswahili mjini Nairobi ilvyo.

2:3:1 <u>LUGHA YA KISWAHILI MJINI NAIROBI</u>

Kwa kuwa mada yetu inazingatia ukiushi unaojitokeza katika matumizi ya kiswahili katika mojawapo ya vitongoji vya mji wa Nairobi, ingekuwa bora pia kuiangalia hali ya lugha ya kiswahili mjini Nairobi kwa jumla. Hali hii yamkini tunaweza kuilinganisha na hali tunayokumbana nayo katika eneo letu la utafiti la Kariobangi South.

Kiswahili kinachotumika katika vitongoji vya mji wa Nairobi hujulikana kwa mchanganyiko wa maneno au sentensi za kiswahili na kiingereza.[7] 'Ukopaji wa msamiati na sarufi ya lugha za kwanza pia hudhihirika. Mchanganyiko huo wote hujitokeza katika "lugha" ya 'kisheng'. Wanapozungumza

wakaazi wa Nairobi, hasa vijana, miundo ifuatayo hujitokeza,

(a) "Karis ana do job Ololo," kwa maana ya, "Kariuki anafanya kazi Kaloleni". Au

(b) "Yeye these days amekuwa mdosi" Ambayo ni, "Yeye siku hizi ametajirika".

Mifano hii inaonyesha dhahiri kwamba wanapozungumza hawajali kutafuta maneno ya kiswahili yanayofaa katika kusema jambo wanalotaka kusema. Kwa mintarafu ya utafiti uliofanywa,[8] ni nadra kwa wazee au watu wazima kutumia 'kisheng'. Kwa hivyo inaelekea kwamba kuna tofauti kati ya Kiswahili cha wazee na "Kiswahili" cha vijana.

Mji wa Nairobi ndio mji mkubwa kuliko yote nchini Kenya. Ndio pia makao makuu ya Serikali ambapo pana idara mbali mbali kama vile Elimu, Utamaduni, Utalii, na nyinginezo. Na kama ilivyo miji yenye sifa hizi, mambo yote mapya kuhusu mila na utamaduni, mitindo ya mavazi, aina ya dansi na hata pia mitindo ya kuzungumza ikianzia hapo huigwa na kusambaa kote nchini. Kutokana na ukweli huu, si ajabu kwamba jinsi lugha ya kiswahili inavyotumika mjini Nairobi inaweza kuathiri matumizi ya lugha ya kiswahili nchini kote kwa jumla.

Hili litakuwa ni tatizo kubwa kwa upande wa matumizi ya kiswahili sanifu. Hasa tunapotilia maanani kwamba

kiswahili kinachopaswa kufunzwa katika shule ni kiswahili sanifu. "Uchafuzi" wa lugha hii utasababisha matokeo mabaya katika mitihani ya kitaifa katika somo la kiswahili. Kwa mwelekeo huu tumejaribu kutoa maelezo kuhusu lugha sanifu ya kiswahili na dhana ya ukiushi kama inavyoweza kujitokeza dhidi ya matumizi ya lugha sanifu katika maongezi ya kila siku.

## 2.4. KISWAHILI SANIFU

Lugha sanifu ni

> "aina ya lugha inayotumika katika maandishi, inayofunzwa shuleni na kufunza wageni wanaotaka kuijua lugha fulani."[9]

Wanaismu wengine kama Trudgill (1974:23) huongezea kwa kusema kwamba lugha sanifu pia ni aina ya lugha inayozungumzwa na wasomi, kutumika katika vyombo vya habari na katika hali nyingine kama hizo. Madai haya yanazusha mjadala kwamba si wasomi wote wanaoizungumza lugha sanifu. Hata wale wanaozungumza katika redio na televisheni, ambavyo ni vyombo vya habari, mara nyingi hufanya makosa ya kilahaja na kilafudhi dhidi ya lugha sanifu.

Aidha lugha inaposanifishwa ni kumaanisha kwamba inatumiwa vile inavyopasa, kwa njia au mbinu zake za sawa-

sawa na kwa njia ya ustadi. Tunapozungumza juu ya kutumia lugha, ya kiswahili, kwa mbinu zake za sawasawa tunatilia maanani kwamba kama lugha yo yote ile, kiswahili kina taratibu zake za kufuatwa katika matamshi, kuunda maneno na pia sentensi. Taratibu hizo ziko katika tajiriba ya kila mtumiaji stadi wa lugha hiyo. Mtu anapozikiuka taratibu hizo, mjuzi wa lugha ya kiswahili sanifu ataelewa wazi kwamba pamefanyika makosa (Taz. Halle na Stevens, 1964).

Mambo kadha wa kadha yalisababisha kusanifishwa kwa kiswahili. Kwa kifupi, tunaweza kusema kwamba juhudi za usanifishaji wa kiswahili zilianza tangu mwaka wa 1925 wakati Gavana wa Tanganyika wakati huo alipoita mtukano huko Dar-es-salaam kuhusu elimu. Haja ya kuchagua lugha moja ya kiafrika katika Afrika Mashariki ilipendekezwa na kiswahili kikachaguliwa kuchukua nafasi hiyo. Hatua hiyo ilikuwa muhimu sana maana hapo ndipo ilipoonekana haja ya kuandika kiswahili kwa lahaja wastani.

Mnamo mwaka wa 1928 Washiriki kutoka Kenya, Uganda, Tanganyika na Zanzibar walikutana mjini Mombasa kushauriana juu ya lugha ya kiswahili. Pakaundwa kamati ya lugha ya kiswahili iliyojulikana kama "Interterriorial language Committee", mnamo mwezi wa Januari mwaka wa 1930. Baadhi ya kazi za kamati hiyo zikawa ni 'kuunda' kiswahili sanifu. Lahaja ya kiunguja ilichaguliwa kwa madai kwamba ndiyo

lahaja ya kiswahili iliyokuwa imeenea sana Afrika Mashariki.

Kamati hiyo baadaye iliunda kamati nyingine ndogo ya uandikaji wa vitabu, "Central Publishing Committee," ili kuchapisha vitabu vya aina moja na kuepusha maadishi mbali mbali. Kamati hiyo pia ilijishugulisha na uandikaji wa kamusi za 'kiswahili - kiingereza' na 'kiingereza-kiswahili'.

Hizi zote zilikuwa juhudi za kutaka kuunganisha lugha ili kuwa na lahaja moja ya kiswahili (sanifu) itakayotumika. Hivi sasa kiswahili ni mojawapo ya lugha zilizoenea sana Afrika. Hutumika kama lugha ya mawasiliano miongoni mwa watu wa asili mbalimbali katika Afrika ya Mashariki na ya kati. Matumizi yake pia yanapatikana katika nchi za Msumbiji, Bukini, Visiwa vya Ngazija na kwingineko.

## 2.5 DHANA YA UKIUSHI

Neno ukiushi linatokana na neno "kiuka". Katika Kamusi ya kiswahili Sanifu, neno hili lina maana ya, "Fanya isivyostahili: vunja sheria" Kutokana na maelezo haya tunaweza kusema kwamba maana yake pia ni "makosa". Katika muktadha wa tasnifu yetu "makosa" haya tunayajadili kutokana na vile yanavyoadhirika katika matumizi ya kila siku tukilinganisha na kanuni za lugha sanifu.

Ni dhahiri kwamba lugha yo yote ile ina sheria zake. Kiswahili sanifu pia kina sheria zake zinazohusu muundo na sarufi yake . Maingilio yo yote yanayoiathiri lugha kimuundo, kisarufi na hata kimsamiati ambayo yanazivunja sheria za lugha hiyo ni ukiushi wa kimatumizi.

Wakati wa kuongea lugha ya kiswahili mzungumzaji anaweza kufanya ukiushi kwa kutumia sauti na miundo ya maneno ya lugha yake ya kwanza katika sentensi za kiswahili. Lugha hutofautiana kimatamshi. Lugha nyingine huwa na sauti fulani zisizopatikana katika lugha ya kiswahili. Kwa mfano, sauti /β/, na /ɣ/ (zilizoko katika kikuyu kwa mfano) hazipatikani katika kiswahili sanifu. Vile vile lugha nyingine hukosa baadhi ya sauti zinapopatikana katika kiswahili sanifu kama vile /ʃ/,/θ/,/S/ na /Z/ (kwa mfano kikuyu hakina sauti) .

Tofauti hizi husababisha kuwepo kwa matamshi au miundo ya maneno yasiyokuwa ya kiswahili sanifu. Kwa mfano ikiwa lugha ya kwanza haina sauti /θ/, mzungumzaji wa lugha hiyo huenda akatamka /Z/ au /ɣ/ badala ya hiyo /θ/. Kwa mfano:-

| <u>Kiswahili sanifu</u> | <u>ukiushi</u> |
|---|---|
| athari | azari au adhari |
| ngozi | ngosi au ngodhi, nk. |

Nao mpangilio wa sauti katika kuunda maneno mara nyingi hutofautiana katika lugha mbalimbali. Hata hivyo baadhi ya lugha za kibantu za Wakenya hufuata mpangilio kama ulivyo wa kiswahili. Ambao ni, 'konsonanti - vokali - konsonanti - vokali' (KVKV), hivi kwamba maneno yote ya kiswahili huishia kwa vokali. Aghalabu hupatikana maneno ya kiswahili yanayotanguliza konsonanti zaidi ya moja zikifuatana. Kwa mfano "mgonjwa", "mpishi", "mpira", na kadhalika.

Kwa kufafanua zaidi pia tunaona kwamba konsonati /d/, kwa mfano, haipatikani katika mwanzo wa neno au mahali pengine katika lugha ya Kimeru isipokuwa iwe imetanguliwa na konsonanti /n/[10]. Kwa sababu hii maneno yote yanayoanza kwa /d/ katika kiswahili huongezwa /n/ kuitangulia /d/ kwa mfano:-

| Kiswahili Sanifu | Ukiuhsi |
|---|---|
| dada | ndanda |
| dawa | ndawa |
| dunia | ndunia |
| deni | ndeni, |
| | na kadhalika. |

Ikiwa lugha ya kwanza na ya pili zinatofautiana katika miundo ya sauti na sarufi basi kunakuwa na shida katika kujifunza lugha ya pili. Yamkini ikiwa tofauti kati ya

lugha hizo ni kubwa, basi vilevile shida ya kujifunza lugha inakuwa kubwa.

Matokeo ya matatizo hayo ni kuwepo na "vilugha' au lahaja mbalimbali za Kiswahili ambazo zinategemea lugha ya kwanza ya kila mzungumzaji. Kwa mfano, neno 'dunga' la kiswahili linaweza kutamkwa 'tunga' au 'ndunga' kutegemea lugha ya kwanza ya mzungumzaji; kama vile Mluhya na Mkikuyu au mkamba. Neno 'ghali' pia huenda likatamkwa 'ngali' na Mkikuyu au 'kali' na Mkamba ambaye hajaimudu lugha hii ya kiswahili kimatamshi.

Katika kutunga sentensi za kiswahili waongeaji wenye athari za lugha za mama mara kwa mara huchanganya viambishi vya kundi la kwanza, la pili, la tisa na la kumi. Badala ya kusema "kuku wale" au "kondoo yule" husema "kuku zile" au "kondoo ile" (mifano zaidi tutaitoa katika kuainishia data).

Ukiushi huu unatokana na ukweli kwamba kiswahili hutumia viambishi vya ngeli za 1 na 2 kwa wanyama ambapo lugha nyingi za kwanza hapa nchini hutumia viambishi vya makundi ya 9 na 10 kwa wanyama.

Katika upande wa msamiati ukiushi pia hudhihirika. Katika kuongea kiswahili watu wengine hutumia meneno kama yanavyotumiwa katika lugha zao za kwanza. Kwa mfano

wazungumzaji wengine hawatofautishi kati ya "kunywa" na "kuvuta". Kwa sababu hii utamsikia mtu akisema, "Fulani anakunywa bangi." Wengine hawatofautishi kati ya ndizi' na'mgomba' kwani katika lugha zao za kwanza wanatumia neno moja (ndizi) kwa mti na matunda yake. Kwa kutofautisha wanapozungumza kiswahili henda wakafanya makosa ya kuuita mti 'ndizi' na matunda yake yakawa 'mandizi'. Pia badala ya kutofautisha kati ya "mpunga," "mchele" na "wali" wazungumzaji wengi hujumlisha vyote wakaviita "mchele".

Makosa kama haya ya kifonolojia, kisarufi' na kimsamiati ndiyo tutakayoyajadili kama ukiushi dhidi ya lugha sanifu ya Kiswahili. Mambo haya tumeyashughulikia katika viwango vya,

(a) Matamshi (fonolojia)

(b) Sarufi (mofolofia na Sintaksia)

(c) Msamiati (Semantiki na leksia).

TANBIHI

1. Nukuu hii imepatikana kutoka kwa utangulizi wa Sapir, E (1969) uk 14-15.
2. Taz Cook (1969).
3. Nukuu kutoka kwa utangulizi wa Dutton, T. E (1976).
4. Maelezo ya Trudgill, (1974) uk 24 -25.
5. Mazrui, A.A (1985) uk. 185.
6. Mbaabu, I, (1978) uk. 10.
7. ibid. " "
8. Nyauncho, O.K. (Tasnifu ya B.A., 1985).
9. Trudgill (1974). uk.23
10. Mbaabu, I, (1978). uk. 56
11. Mnyampala, M., na Chiraghdin, S. (1977) uk.54.

## SURA YA TATU

### 3.0 UKIUSHI KATIKA MAONGEZI YA LUGHA YA KISWAHILI

### 3.1 UTANGULIZI

Kulingana na maelezo ambayo tumeyatoa katika sura ya kwanza, lengo letu limekuwa ni kutafiti juu ya ukiushi unaopatikana katika maongezi ya kila siku dhidi ya lugha sanifu ya Kiswahili baina ya wakazi wa Mtaa wa Kariobangi South. Katika mtaa huu tumeona kwamba mnaishi watu wenye asili tofauti tofauti na wanazungumza lugha tofauti za kwanza. Madhumuni hasa ya utafiti wetu yamejikita katika sehemu mbili;

(a) Kuyaainisha makosa yote ya ukiushi unaojitokeza katika mazungumzo ya wahusika dhidi ya lugha ya Kiswahili sanifu; katika viwango vya kifonolojia, kisarufi (mofolojia na sintaksia) na kimsamiati (leksia na semantiki), na

(b) Kujaribu kuelezea, kulingana na uchunguzi wetu, mambo yanayosababisha makosa hayo; tukizingatia hasa lugha za kwanza wanazoziongea wahusika wanaofanya makosa hayo.

Kwa kufanya hivyo, kwanza tumeyanakili makosa yaliyojitokeza katika mazungumzo ya kawaida kwa kutumia mbinu ya 'mhusika - mtafiti' katika muktadha wa mazungumzo ambapo tumechukuwa nafasi ya mhusika katika

mazungumzo badala ya kuwa tunawahoji wahusika wetu moja kwa moja. (Taz. mbinu za utafiti, sehemu 1.8).

Mazungumzo tumeyarekodi katika kanda za vinasa-sauti. Imetubidi kufanya uteuzi wa data yetu ili kuweza kupata data mwafaka ambayo inafaa katika kuiwasilisha kazi yetu. Sababu moja ya kufanya hivi ni kwamba tumeweza kuepukana na kurudia - rudia aina moja ya makosa yanayojitokeza mara kwa mara. Kwa mfano, makosa mengi sana tuliyoyapata katika utafiti wetu yalikuwa makosa ya kifonolojia. Kati ya hayo, takriban nusu yake yanahusu ukiushi katika matumizi ya fonimu /r/ na /l/ kulingana na miktadha mbalimbali. Ndiposa imetubidi kuteua miktadha michache tu katika kuiwasilisha kazi ya utafiti wetu.

Tumenuia pia kubainisha aina nyingi tofauti tofauti ya makosa katika data tuliyoipata, badala ya kuwa na mifano mingi inayoelezea jambo moja (aina moja ya ukiushi).

Uteuzi huu tumeufanya kulingana na ujuzi wetu wa lugha ya Kiswahili sanifu. Kama wanovyosema Halle na Stevens (1964), kwamba,

"Msikilizaji wa lugha fulani, akiwa anaifahamu lugha hiyo, huzitambua arki za kifonolojia, kileksia na kisarufi katika usemi wo wote kwa njia ijulikanayo kama 'uchanganuzi kwa uunganishaji' (Tafsiri yetu).

Kwa njia hii na pia kwa elimu yetu tuliyonayo kuhusu sarufi ya Kiswahili sanifu, tumeweza kuyatambua na kuyabainisha makosa ya kifonolojia, kisarufi, na kileksia na kimaana katika maongezi ya wakazi wa Mtaa wa Kariobangi South, mjini Nairobi.

Kwa mintarafu ya utafiti wetu, inaonekana dhahiri kwamba ukiushi katika Kiswahili kinachozungumza katika mtaa huu unatokana na hoja mbili zinazoingiliana;

(a) Makosa mengi, hasa yale ya kifonolojia, yanatokana na athari za lugha za kwanza za mzungumzaji, na

(b) athari za kimazingira, ambapo lugha ambayo mtu 'amejifunza', tayari ilikuwa na ukiushi wake aliouiga 'kikasuku'. Athari hizi za kimazingira zinajitokeza sana katika makosa ya kisarufi na kimsamiati. Kama inavyodhihirika na uchanganuzi wa data).

Matokeo ya makosa haya ni kuweko kwa aina za 'pijin (vilugha) za Kiswahili dhidi ya lugha ya Kiswahili sanif Makosa ya kifonolojia yanajitokeza katika lafudhi wakati m anapozungumza Kiswahili kilichoathiriwa sana na lugha ya ya kwanza. Hii inakuwa ni lafudhi ambayo haiambatani matamshi ya Kiswahili sanifu. 'Pijini' zinahusu viwar ambapo miundo ya kimofolojia na kisintaksia ya Kiswahi sanifu inatupiliwa mbali na mzungumzaji na badala ya akatumia miundo iliyosahilishwa. Kwa mfano Kiswahili ki sifa ya kuwa lugha ambatanishi ambapo sentensi nzima, k mfano, inaweza kuwakilishwa na neno moja. Kama vi 'Hajaniambia' (sentensi). Katika neno hili [Ha] kiambishi cha kukanusha kinachosimamia 'nomino' ambayo katika sentensi. Silabi [ja] ni kiambishi cha wakati [ ni objekti na [ambia] ni kitenzi katika hali ya kutend Kwa hivyo katika hilo neno moja la Kiswahili tumep sentensi mzima yenye sifa zote za sentensi kamilifu; amb ni sabjekti, kiambishi cha wakati, objekti na kiten Katika kusahilisha mazungumzo mazungumzo mzungumzaji amb hajaimudu lugha sanifu ya Kiswahili husema;

'Yeye hajaambia mimi'. (Bw. Oloo)

Aghalabu ukiushi wa aina hii unatokana na mzungumz ambaye lugha yake ya kwanza ina miundo tofauti kimofolojia na kisintaksia ikilinganishwa na ile ya lugha Kiswahili. Mzee Oloo ambaye ni Mjaluo aliyehusika kat

utafiti wetu ndiye aliyeliwasilisha kosa hilo ambalo tumelitaja hapo juu. Inaelekea kwamba miundo ya lugha ya kijaluo (Kinailotiki) imetofautiana na miundo ya lugha ya Kiswahili ndiposa mzungumzaji anafanya kosa kama hili la kimuundo.

Katika utafiti wetu pia tumeona kwamba athari za kilafudhi zinaambatana na makosa katika matumizi ya lugha. Hivi ni kusema kwamba wahusika ambao lafudhi zao au matamshi yao yameathiriwa sana na lugha zao za kwanza, ndio wanaofanya makosa katika kutumia miundo ya lugha. Wale wanaozungumza Kiswahili kilichosanifika kwa kiwango kikubwa, ni wale ambao hawadhihirishi matamshi ya lugha zao za kwanza wanapozungumza Kiswahili (kwa mfano, katika matamshi ya Bw. Nzioka na Bw. Kipkorir ambao ni wahusika katika utafiti wetu) au athari hizo zinatokea kwa nadra sana.

Katika sura zinazofuata, tumezijadili hoja zinazojitokeza kuhusu viwango vya ufasaha wa matumizi ya lugha na kuainisha ukiushi unaojitokeza, kulingana na viwango mbalimbali vya lugha, kama tulivyoupata kutokana na utafiti wetu.

### 3.1.2 VIWANGO VYA UFASAHA WA LUGHA

Kwa mintarafu ya utafiti wetu tunaweza kuwagawanya wazungumzaji wa Kiswahili kulingana na 'ufasaha' wao wa lugha ya Kiswahili kwa namna hii;

(a) Wenye kuongea 'Kiswahili cha kuomba maji', ambacho ni Kiswahili cha kiwango cha chini sana. Wengine wao hukiri kwamba wanajua 'Kiswahili moja-moja'. Wanapozungumza wanakichanganya sana na lugha zao za kwanza na mara nyingine (kwa waliosoma) hutumia msamiati na miundo ya kisarufi ya Kiingereza. Wahusika ambao wanazungumza Kiswahili hiki ni Bw. Obiero mwenye umri wa miaka 52 ambaye ni Meneja wa benki. Yeye huongea Kiswahili akitumia maneno kadha ya Kiingereza na miundo ya kisarufi ambayo si ya Kiswahili fasaha. (Taz. uchambuzi wa data). Mwingine mwenye kuzungumza 'Kiswahili cha kuomba maji' ni mama Kamau, pia mwenye umri wa miaka 52 ambaye ameathiriwa sana na lugha yake ya kwanza hata anatumia miundo ya lugha ya Kikuyu akiwa anaweka 'neno moja moja' la Kiswahili katika mazungumzo yake.

(b) Wenye kuongea 'Kiswahili nusu-nusu' ambao Kiswahili chao kimeathiriwa na lugha zao za kwanza (na pia Kiingereza). Ingawa wanakifahamu na kukiongea Kiswahili wanakiongea 'vibaya' kwa sababu ya athari hizo. Viwango vya ujuzi wa lugha vinatofautiana kwani kuna wale watakaozungumza 'Kiswahili kidogo-kidogo' kama

vile Bw. Hassan na Bw. Oloo na wale ambao ufasaha wao ni wa hali ya juu zaidi ukilinganishwa na hawa. Zaidi ya nusu ya wahusika wetu kwa jumla walikuwa katika kundi hili, ingawa pia katika viwango vinavyotofautiana. Tofauti hizi tumeziainisha katika kuichambua data yetu.

(c) Wenye 'kuongea Kiswahili vizuri'. Kama tulivyokwisha kuona hapo awali, mzungumzaji hawezi kuitumia lugha kwa ukamilifu wote wa ufasaha. Usanifu wa lugha (ya kimaongezi) kwa ujumla ni dhana ya kidhahania. Mzungumzaji ye yote yule awe amemakinika katika matumizi ya lugha jinsi gani sharti awe na athari zake au ukiushi wake wa kibinafsi (Taz. Max Black, 1965:75).

Hata hivyo, tunapotaja 'kuongea Kiswahili vizuri' tunamaanisha kwamba ni kwa matumizi ya ufasaha mkubwa. Katika utafiti wetu, wahusika waliodhaihirisha ufasaha mkubwa katika matumizi yao ya lugha ni Bw. Nzioka na Bw. Kipkorir ambao walisalitiwa tu na makosa machache ya kimatamshi ambayo hayakujitokeza katika miktadha mingine katika mazungumzo yao. Hata hivyo walitumia miundo 'fasaha' ya kisarufi na msamiati.

Inasemekana (Trudgill, 1974) kwamba kwa kawaida mtu aliye na elimu ya kiwango cha juu hujitahidi kuitumia lugha 'vizuri' kuliko yule ambaye ama hajasoma au kiwango chake

cha elimu ni cha chini. Kwa kweli hoja hii haikudhihirika kikamilifu katika utafiti wetu. Kwa mfano Bw. Obiero ambaye alisoma hadi chuo kikuu alifanya makosa mengi sana katika maongezi ya Kiswahili. Kwa maoni yetu, ikiwa hoja hii inakubaliana na lugha nyinginge kama vile Kiingereza, haina mashiko kuhusiana na lugha ya Kiswahili. Si jambo la kuukatiwa kauli ya kijumla, eti waliosoma huongea lugha fasaha.

Umri huathiri matumizi ya lugha ya Kiswahili kutokana na ukweli kwamba watoto mara nyingi hutumia lugha kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe bila hata kuzizingatia kanuni za lugha. (Taz. Nyauncho, O. K.; 1985, tasnifu ya B.A). Hili pia ndilo jambo mojawapo lililosababisha kuwepo kwa 'vilugha' vya 'sheng' ambayo ni lugha inayotumiwa na watoto katika baadhi ya mitaa ya jiji la Nairobi hasa katika sehemu ya mashariki mwa jiji hili. Jinsi Kiswahili kinavyotumiwa katika maongezi haya ni tofauti kabisa na kaida za Kiswahili sanifu. Huu ni ukiushi wa namna yake ambao hatukukusudia kuujadili hapa.

Fauka ya hayo tuliyoyataja kuhusu viwango vya ufasaha wa lugha, tunapata pia 'misemo' inayojitokeza kuhusu matumizi ya lugha ya kimaongezi ambayo yanadhihirisha athari za lugha za mama (hasa katika upande wa fonolojia na sintaksia). Watu wenye hisia za kikabila wamejitokeza na

misemo ya 'kuzungumza Kiswahili kama Mkamba', 'kuzungumza Kiswahili kama Mjaluo', na kadhalika. Hili lenyewe ni thibitisho kwamba lugha ya Kiswahili imekumbwa na ukiushi mkubwa katika matumizi yake, na kama tuliyokwishataja ukiushi huu unategemea athari za lugha tofauti tofauti za kwanza.

Katika sura zinazofuata tunazumgumzia kuhusu ukiushi huo katika viwango vitatu vikuu. Viwango hivi ni kiwango cha fonolojia, kiwango cha sarufi, na kiwango cha msamiati na maana.

## 3.2 UKIUSHI KULINGANA NA KIWANGO CHA FONOLOJIA

Kuhusu ukiushi wa kifonolojia, dhana hii tunaijadili kwa maana ya matamshi katika maongezi ya lugha ya Kiswahili. Hii ni kwa sababu tasnifu hii inashughulikia ukiushi katika matumizi ya lugha kulingana na miktadha ya kimaongezi. Kwa hivyo tunapozungumzia kuhusu fonolojia, kwa hakika tutakalo lijadili ni swala la kimatamshi, jinsi fonimu za zinavyojitokeza (au kutojitokeza) kama sauti katika mazungumzo.

Katika kiwango hiki cha fonolojia tumezigawanya hoja zetu mara mbili. Tunazungumzia kuhusu ukiushi wa ki-vokali na kisha tuzungumzie ukiushi unaohusu matumizi ya konsonanti.

Lugha ya Kiswahili sanifu ina jumla ya vokali tano. Vokali hizi ni /a/, /e/, /i/, /o/ na /u/. Kikamba na Kikuyu ambazo pia ni lugha za Kibantu zina vokali mbili zaidi ya hizi. Vokali hizo ni /ĩ/ na /ũ/ ambapo jumla huwa ni vokali saba katika lugha hizo. Kutokana na utafiti wetu, tumeona kwamba sauti hizi za ziada ambazo haziko katika lugha ya Kiswahili mara nyingi huathiri matamshi ya watu wanaozungumza lugha hizi (kama lugha za kwanza) katika matumizi yao ya lugha ya Kiswahili. Kwa mfano sauti /u/ ya Kiswahili huteremshwa kifonetiki na kuwa /ũ/ ya Kikuyu na Kikamba. Kwa kufafanua zaidi tumetoa mifano hapa chini;

(A) <u>KUBADILISHA VOKALI</u>

a) <u>Matumizi ya fonimu /ũ/ badala ya /u/</u>

<u>Kwa mfano</u>: mwarimũ kwa maana mwalimu.

<u>Sentensi</u>: (i) "Mwarimũ wao amewapea kasi ya hesabu." (Mama Njuguna).

(ii) "Dimũ tunausa shirigi." (Mama Njuguna). Akimaanisha: "Tunauza ndimu kwa bei ya shilingi moja."

b) <u>Fonimu /i/ badala ya /e/</u>

k.m. 'mkati badala ya mkate'.

Sentensi: (i)"Bado hujanipatia pesa za mkati." (Peter)

c) Fonimu /ĩ/ badala ya /i/

k.m. 'Dukanĩ kwa maana ya dukani'.

Sentensi: (i) "Kwishatuma yeye ndukainĩ." (Mama Kamau).

(B) KUONGEZA VOKALI MAHALI ZISIPOHITAJIKA

(a) Kuongeza vokali /u/ baada au kabla ya /m/

k.m. 'mutu muzuri' badala ya mtu mzuri'

Sentensi: (i) "John ni mutu muzuri, yeye anafanya kazi muzuri." (Muturi). au

- "umbwa" badala ya "mbwa", na
- "umbu" badala ya" mbu",

(ii) "Umbwa sa Njiriri sililia sana usiku." (Bi. Maranya).

(iii)"Kunakuwa na umbu mingi sana usiku." (Kimeu).

(c) Kuongeza vokali /i/

k.m.inje badala ya nje.

inchini badala ya nchini.

Sentensi: (i) "Hii inchi imekuwa mbaya kwa waisi." (Odhiambo).

(ii)"Akinyi funga milango ya inje." (Bi. Obiero).

(d) <u>Kudondosha vokali /i/</u>

k.m. "ngia' badala ya "ingia".

"sirini" badala ya "ishirini".

Sentensi: (i) <u>"ngia</u> kwa bas na kupatiana siling sirini." (Onyango).

(e) <u>Kuongezea vokali /o/</u>

k.m. "ongoja" badala ya "ngoja".

<u>Sentensi</u>: "Ongoja kidogo nimalise hii kasi" (Bi Obiero).

Makosa yanayofanyika katika (A) kubadilisha vokali na (B) kuongeza vokali /u/ katika matamshi ya Kiswahili yametokana na wazungumzaji wa lugha za Kikuyu, Kimeru, Kikisii na Kikamba, kama tunavyoona katika sentensi hizo za mifano. Uchunguzi ulionyesha kwamba wametumia mipangilio ya sauti kama inavyopatikana katika lugha zao za kwanza. Kwa mfano, katika Kimeru 'mtu' huitwa 'muntu' na katika Kikuyu ni 'mundu'. Kwa hivyo wanaozungumza lugha hizi wanaathiriwa na mpangilio huu wa sauti na badala ya 'mtu' katika Kiswahili wanatamka 'mutu'.

Kulingana na makosa tuliyoyapata ya kuongeza vokali /o/ kama viambishi na kudondosha vokali /i/ mwanzoni wa maneno, utafiti umeonyesha kwamba makosa haya yanatokana na waongeaji wa Kiluo. Lugha ya Kiluo ni lugha ya Kinailotiki.

Tofauti na lugha za Kibantu zinazopatikana hapa Kenya, lugha za Kinailotiki haziambatani kimuundo wala Kisintaksia na lugha ya Kiswahili. Kwa hivyo makosa ya kuongezea au kudondosha sauti kama haya aghalabu yanatokana na tofauti hizo.

Licha ya makosa hayo yanayohusu vokali tulipata makosa mengine yanayotokana na matumizi ya konsonanti.

UKIUSHI KUHUSU KONSONANTI

Katika kulichunguza swala la ukiushi unaotokana na matumizi ya konsonanti katika maongezi, makosa mengi tofauti yalijitokeza. Makosa yenyewe ni:

(a) Kuongeza fonimu mahali isipohitajika

i) /h/ kabla ya vokali.

k.m. ha(n)dabu - adabu.

Sentensi: "Waizi wameshikishwa handabu." (Kimeu)

"Kioko hamekwenda shule." (Bi. Nzioka).

ii) Kuongeza /n/ kabla ya /d/

k.m. "ndunga" - dunga.

"ndunia" - dunia.

"ndanda" - dada.

Sentensi: "Wakola walimundunga na kisu." (Kimeu)

"Mabo ya ndunia inapotesa watoto yetu." (Mama Roda)

"Ni kama file ndanda Mbitres alifyosema." (Jeremiah)

iii) Kuongeza /m/ kabla ya /b/

k.m. "Mbakora" - bakora.

"Mbahari" - bahari.

"Mbasi" - basi.

Sentensi: "Akikuja piga yeye na mbakola." (Baba Mwangi)

"Ni mbahati musuli guo yako iko tayari." (Bi. Njuguna)

"Utapada tu mbasi sa Ndandola." (Mama Wambua)

iv) Kuongeza /n/ kabla ya /g/

k.m. " ngazeti" - gazeti.

"ngunia" - gunia.

"ngodoro" - godoro.

Sentensi: "Nipatie ngaseti ya 'Nation'." (Bw. Maranya)

"Nimenunua ngunia moya (ya mahindi) silingi mia sita." (Mama Wambua)

"Kunauswaghwa mangondolo huko Industrio." ("Customer"). Maana: Magodoro huuzwa huko 'Industrial Area'.

v) Kuongeza /n/ kabla ya /j/

k.m. "njokoo" - jogoo.

"njaa" - jaa.

"njali" - jali.

Sentensi: "Nipatie unga ya njokoo." (Bi. Nzioka)

"Matakataka imenjaa huko kwa chokoraa." (Kimeu)

"Usinjari hii (nyama) ni ya reo". (Baba Mwangi)

vi) Kuweka kiambishi /m/ kisichokuwepo

k.m. "mambia" - ambia.

"manasema" - anasema.

"manaimba" - wanaimba.

Sentensi: "Wewe na mambia mimi namna gani?" (Bw. Obiero)

"Manasema manataka itunguru." (Mama Kamau). Kwa maana ya; "Anasema anataka (kuuziwa) vitunguu."

"Watu ya kwaya manaiba musuri." (Mama Roda)

Katika sehemu ya (a), utafiti umeonyesha kwamba kosa hili latokana na wazungumzaji wa lugha ya kikamba. Tumechunguza tukaona kuwa katika matamshi ya lugha hii ya Kikamba hakuna sauti /h/ kwa hivyo wazungumzaji wanapokutana na sauti hiyo katika kuongea Kiswahili au lugha nyingine yenye sauti hiyo mara nyingi hutatizika. Wanaiweka sauti hiyo mahali isipohitajika na kuidondosha mahali inapohitajika.

Kosa la kutanguliza /n/ kabla ya /d/ katika matamshi pia limeonekana kwamba latokana na sababu za athari za lugha za kwanza za wazungumzaji wa asili ya Kikuyu, Kikamba, Kimeru na Kembu, kama utafiti wetu ulivyoonyesha. Aghalabu katika lugha hizi sauti /d/ hutangulizwa na /n/ katika matamshi. Tumeona pia kwamba wanaofanya kosa la kuongezea /n/ kabla ya /d/, pia hufanya kosa la kuongezea /m/ kabla ya /b/ na /n/ kabla ya /j/ na /g/. Haya ni makosa yanayofanywa na wazungumzaji wa asili ya Kibantu kuliko wanailotiki.

Kuhusu kosa la kuongezea /m/ kabla ya /a/, yaonekana kwamba kuna yale yanayofanywa na Wanailotiki na yale yanayofanywa na Wabantu. Kwa mfano, neno 'mambia' latokana na mzungumzaji wa asili ya kiluo (kinailotiki). Ni vigumu kulipata kwa mzungumzaji wa asili ya kibantu.

(b) Udondoshaji wa fonimu

Kosa la udondoshaji wa fonimu linahusiana na lile la kuongezea kwa fonimu mahali isipohitajika. Utafiti wetu umeonyesha kwamba wale wazungumzaji wanaoongezea /h/ kabla ya vokali katika matamshi yao, ndio wanaoidondosha fonimu hiyo. Kwa mfano kama tulivyokwisha kuona, wazungumzaji ambao lugha zao za kwanza ni Kikamba ndio wanaodhihirisha matatizo haya katika matamshi yao. Uchunguzi zaidi kutokana na utafiti umeonyesha kwamba katika lugha ya kikamba sauti hii /h/ haipo. Kwa hivyo basi, ni dhahiri kwamba makosa haya wanayoyafanya katika matamshi ya Kiswahili yanatokana na athari ya lugha yao ya kwanza. Mifano ya udondoshaji kutokana na data yetu ni hii;

i) Udondoshaji wa sauti /h/ inayotangulia vokali

k.m. "abari" - habari.

"ma'alakwe" - maharagwe.

"ma'indi" - mahindi.

"esabu" - hesabu.

Sentensi: "abali yako mama Chake?" (Kimeu)

"Na usisa'au a'adi ni ndeni." (Bi. Nzioka)

"Pima kilo mbili sa ma'alakwe." (Mama Wambua)

"Amekosea 'esabu." (Mama Wambua).

ii) Udondoshaji wa fonimu /m/ na /n/ (Sauti za nasali)

Fonimu /m/ hudondoshwa katika matamshi hasa inaokuja kabla ya fonimu /b/, kulingana na jinsi tulivyoona katika utafiti wetu. Nayo fonimu /n/ imeonekana kwamba inadondoshwa inapotokea kabla ya fonimu /g/, /d/ na /j/ katika matamshi ya Kiswahili.

k.m. 'iba' - imba.

'mabo' - mambo.

'kibia' - kimbia.

Sentensi: "Watu ya kwaya manaiba musuri." (Mama Roda)

"Mabo ya ndunia inapotesa watoto yetu." (Mama Roda)

"Watu ya 'kajo' warikunja tukakibiria huko." ('Customer')

('Watu ya kajo' ni wafanyi kazi ya 'City Council (Commission).

'pelemede' - peremende.

'mugu' - mungu.

'kweda' - kwenda.

Sentensi: "Mtoyi (mtoto) si useme unataka pelemede." (Mwangi)

"Mabo ya Mugu ni musuli kwa watoto." (Mama Roda).

"Amekweda soko." (Kariuki)

Sentensi: "Utanunua jughu?" (Mama Kamau)

"Hii ng'obe ilishijwa reo." (Muturi)

Kama inavyoonekana kutokana na data yetu, makosa haya yametokana na wazungumzaji wa lugha za Kikuyu na Kimeru. Hivi si kusema kwamba wengine hawafanyi makosa haya. Tumeona kwamba makosa kama haya pia yanatokana na wazungumzaji wengine wa lugha za Kikamba, Kiembu, na Kikisii. Hatukuweza kuyinisha makosa yote hapa bali tumetoa tu makosa machache ya kuwasilisha yale makosa mengi tuliyoyapata ya aina hii.

(c) <u>Kubadilisha fonimu</u>

Kwa mintarafu ya utafiti wetu, tumeona kwamba wapo wazungumzaji wengine ambao hawatofautishi kati ya sauti /t/ na /d/ au /k/ na /g/, na /p/ na /b/. Wazungumzaji hawa (wanaozungumza lugha za kwanza za Kiteso, Kibukusu (Kiluhya na Kikamba) husababisha ukiushi katika matamshi yao ya Kiswahili. Licha ya makosa haya, kuna pia makosa mengine ambapo sauti za kawaida za Kiswahili zinatamkwa tofauti na jinsi zinavyokusudiwa katika Kiswahili sanifu. Sauti hizi ni kama vile /gh/ badala ya sauti /g/, na /y/ badala ya sauti /j/, kama zinavyotamkwa na wahusika wetu wengine wa asili ya Kikamba(km. mama Wambua na Bi. Nzioka).

Hapa tunatoa mifano michache ya kuonyesha mabadiliko hayo ya sauti jinsi zilivyotamkwa na baadhi ya wahusika katika utafiti wetu.

i) <u>/t/ badala ya /d/</u>

k.m. "kitoko" - kidogo.

"muta" - muda.

<u>Sentensi</u>: "Ngochea <u>muta</u> <u>kitoko</u> nitamalisa." (Mama Shem)

Katika mfano huu tunaona kwamba kosa hili linatokana na mzungumzaji wa lahaja ya kiluhya ambayo ni kibukusu. Makosa ya aina hii pia tuliyapata katika mazungumzo ya Bw. Ibrahim, Mary na Lukalo ambao pia ni waongeaji wa lahaja za kiluhya. Hayo pia yanahusu mabadiliko ya sauti kama haya ya Mama Shem lakini katika miktadha na sajili tofauti.

ii) /k/ mahali pa /g/

k.m. "kundua" - gundua.

"nduku" - ndugu.

Sentensi: "Nimekunduako 'style' mpya ya kufunga 'piece." (Mary)

"Huyu ni nduku yako? Amekufanana!" (Mama Shem)

"Ninakaanga na nduku yangu uko Uruma." (Kimeu).

Mifano hii imeonyesha kwamba makosa ya aina hii yametokana na wazungumzaji wanaoongea lugha za kwanza za kiluhya na kikamba. Tumechunguza na kuona kwamba kuna ukosefu wa sauti /g/ katika lahaja na lugha wanazozizungumza wahusika hawa na ni kwa sababu hii ambapo matamshi yao ya lugha ya Kiswahili yanaathirika.

iii) /p/ mahali pa /b/

k.m. "pipi" - bibi.

"pipilia" - Bibilia.

Sentensi: "Ile mzee iko pipi mbili." (Ibrahim)

"Niliwachako pipilia yangu nyumbani." (Mama Shem)

Matamshi ya aina hii yamejitokeza katika matamshi ya wahusika wetu wanaozungumza lahaja za lugha ya kiluhya. Kwa hivyo inaelekea kwamba yanatokana na athari za lugha yao ya kwanza.

iv) /ch/ mahali pa /j/

k.m. "Chembe" - jembe,

"Kichana" - kijana.

Sentensi: "Patia mimi chembe yako." (Mama Jane)

"Kichana yake amemfwanana kabisa." (Mama Shem)

Mama Jane ni mteso na Mama Shem ni Mubukusu (Mluhya). Katika kuwahoji baada ya utafiti wetu wa kutafuta data, walituambia kwamba sauti /j/ haipatikani katika matamshi ya lugha zao. Kwa hivyo tunaweza kusema kwamba ukosefu huu wa sauti hii ndio

unaosababisha ukiushi wa matamshi wanapoongea lugha ya Kiswahili.

v) <u>/f/ au /b/ mahali pa /v/</u>

k.m. "fiatu" - viatu.

"mfua" - mvua.

"mwafuli" - mwavuli; au

"biatu" - viatu.

"mbua" - mvua.

<u>Sentensi</u>: "Umefaa <u>fiatu</u> yako namna kani?" (Kimeu)

"Nimesaau <u>mwafuli</u> na iko mfua." (Mama Wambua)

"<u>Biatu</u> yako nakwisakwisa sababu ya <u>mbua</u>." (Oloo)

Oloo hapa anasema kwamba, "viatu vyako vimeharibika (vimekwisha) kwa sababu ya mvua."

Makosa haya, tumegundua, kutokana na uchunguzi wetu, kwamba yanatokana na kule kukosekana kwa sauti /v/ katika matamshi ya lugha hizi. Ndiposa wanapozungumza lugha ya Kiswahili wanafanya makosa haya ya kubadilisha sauti kwa kuiweka ile inayopatikana katika lugha zao ambayo imekaribiana (kifonetiki) na hii /v/ ya Kiswahili.

vi) /s/ mahali pa /z/ au /sh/ (/tʃ/)

k.m. "Saiti" - zaidi.

"mbusi" - mbuzi; au

"samba" - shamba.

"sinda" - shinda.

Sentensi: "Isi mbusi sa waria nitasigonga." (Kimeu)

"Watoto wanaselewa saidi na wanachesachesa apo inje." (Beatrice)

Wahusika hawa (Kimeu na Beatrice) ni wakamba. Aghlabu matamshi haya yanatokana na athari za lugha yao ya kwanza ambapo sauti hizi zinawatatiza kulingana na jinsi zinavyotumika katika lugha ya Kiswahili.

Sentensi: "Samba yetu ni kubwa." (Anna)

"Nani amesinda 'Safari Rally?" (Oduori)

Kulingana na utafiti wetu, tumeona kwamba sauti /sh/ inayopatikana katika Kiswahili huwatatiza wahusika wanaozungumza lugha za Kikamba, Kiembu, Kimeru, Kikisii, Kiteso na Kiluo. Katika mifano hii, wahusika hawa wawili,

Anna ni Muembu na Oduori ni mluo. Makosa yao ya kimatamshi ya sauti hii yametokana na kutokuwepo kwa sauti hii katika lugha zao za kwanza (Kulingana utafiti wetu).

vii) <u>Sauti /gh/ mahali pa /k/ au /g/</u>

k.m. "ghwagu" - kwangu.

"tagha" - taka.

"dughu" - ndugu.

<u>Sentensi</u>: "Dughu yagu anakaaga ghwagu." (Baba Mwangi)

"Mimi natagha ghwenda ghwa soko." (Bi. Kipkorir)

Kama vile tulivyokwisha kuona katika mifano ya awali, makosa mengi ya kimatamshi yanatokana na ama kutokuweko kwa sauti hizo katika lugha za kwanza za wazungumzaji au tofauti katika kuzitamka sauti hizo. Kwa mfano, jinsi sauti /b/ inavyotamkwa katika Kiswahili sanifu ni tofauti na vile inavyotamkwa katika Kikuyu. Vile vile sauti /d/ hutamkika kwa njia tofauti katika lugha hizi mbili. Moja hutamkwa kama sauti ya dentali (ya Kiswahili) na nyingine hutamkwa ulimi unapogusa tuta la neno masine (alveola ridge).

Mifano tuliyoitoa kuhusu matamshi ya /k/ na /g/ kubadilishwa yanatokana na sababu kwamba katika Kikuyu (Mfano,Baba Mwangi) na Kinandi (Mfano Bi. Kipkorir) sauti hizi za Kiswahili hazipatikani na kujitokeza katika matamshi jinsi zinavyojitokeza katika matamshi ya Kiswahili.

viii) /r/ mahali pa /l/ na /l/ mahali pa /r/

k.m. "kira" - kila.

"mwarimu" - mwalimu; au

"laa" - raha.

"loo" - roho.

"luka" - ruka.

Sentensi: "Kira njumapiri watoto wakunje mapema kwa kanisa." (Jeremiah)

"Mwarimu wao amewapea kasi ya hesabu." (Mama Njuguna)

"Niliposikia neno la Bwana loo yangu ilisikia laa sana na nikalukaluka." (Mama Wambua)

Kosa la kubadilishana kwa sauti hizi linatokana na sababu kwamba katika lugha hizi, Kikamba, Kikuyu, Kimeru na Kiembu, mojawapo ya sauti hizi hazipo. Kwa mfano Kikamba kina sauti /l/ lakini hakina sauti /r/; nacho Kikuyu kina sauti /l/. Tofauti hizi ndizo zinazosababisha makosa kama haya hapa juu ambapo wazungumzaji wanakanganyika kwa kutotambua ni wapi watakapotumia sauti gani kati ya hizi mbili.

ix) <u>/y/ au /z/ mahali pa /j/</u>

k.m. "mayani" - majani.

"kuya" - kuja, au

"nziani" - njiani.

<u>Sentensi</u>: "Iko mayani ya chai?" (Bi. Nzioka)

"Leo nimekuya kukutembelea." (Bi. Nzioka)

"Tulikutana na yeye nziani." (Bi. Nzioka)

"Katika inzili ya Luka...." (Beatrice)

Wahusika hawa huzunguma lugha ya Kikamba kama lugha yao ya kwanza. Uchunguzi umeonyesha kwamba katika lugha hii hakuna sauti /j/ kama ilivyo katika Kiswahili. Kwa hivyo katika matamshi yao wanaathiriwa na lugha yao ya kwamza na kufanya makosa katika Kiswahili.

## 3.3 HITIMISHO

Kwa kweli makosa yanayofanyika kuhusu ubadilishanaji wa sauti katika matamshi ni mengi mno. Ni vigumu kuyachanganua yote katika kazi ya tasnifu kama hii ambayo licha ya kuwa imewekewa mipaka ya kiwakati ya kuikamilisha, inanuia pia kuaungalia ukiushi mwingine katika viwango vya kisintaksia, na kileksia na kisemantiki. Ni nia yetu kwamba haya tuliyoyazungumzia kuhusu makosa ya kifonolojia yanatosheleza katika kuelezea juu ya tukio la ukiushi unaopatikana katika maongezi ya kila siku ya wakazi wa mtaa wa Kariobangi South katika mazungumzo yao kwa lugha ya Kiswahili.

Katika sura ya sita tumependekeza kwamba swala hili la ukiushi linaweza kuchambuliwa kwa undani na kamilifu zaidi ikiwa mtafiti atakichunguza na kukijadili kipengee kimoja wapo cha lugha katika utafiti wake. Kwa mfano mtafiti achunguze tu kuhusu ukiushi katika kiwango cha fonolojia, au katika kiwango cha mofolojia, na kuchanganua makosa mengi zaidi kuliko kuzungumzia juu ya sehemu zote kwa pamoja katika kazi kama hii.

Hata hivyo, kama lilivyo lengo letu, katika sura ifuatayo tunazungumzia kuhusu matokeo yetu ya utafiti katika sehemu ya mofolojia na sintaksia. Si kusudi letu, katika tasnifu hii kuzungumzia kuhusu fonimu-bandikizi ('Suprasegmental phonemes') kama vile kiimbo na mkazo.

Sehemu hii ya lugha inahitaji ujuzi wake kuhusu taaluma ya viimbo na mkazo na haitawezekana kushughulikiwa katika tasnifu hii kwa sababu ya muda tulionao na mambo yote kwa jumla tunayoyashughulika.

# SURA YA NNE

## 4.0. UKIUSHI WA KISARUFI

### 4.1 UTANGULIZI

Tumezungumiza juu ya makosa ya kimatamshi yanayopatikana katika maongezi ya kawaida ya wakazi wa mtaa wa Kariobangi South. Katika kuelezea ukiushi unaotokea katika matumizi ya lugha haitoshi kuzungumzia tu upande wa matamshi. Mofolojia na sintaksia pia ni sehemu muhimu sana katika lugha. Tutavijadili vipengee hivi vya lugha chini ya mada ndogo ya 'ukiushi wa kisarufi. M.C. Kapinga (1983:2) ameifafanua maana ya neno sarufi kuwa sehemu,

> '...inayoshughulikia jinsi zana za lugha zilivyoumbwa na kupangiliwa katika mifumo mbalimbali".

Kama tulivyokwishataja hapo juu, sehemu hii inayoshughulikia ukiushi katika kiwango cha sarufi tutaigawanya mara mbili. Kwanza tutayashughulikia makosa ya kimofolojia na kimofofonemiki kisha tutayajadili makosa ya kisintaksia kama tulivyoyapata katika utafiti wetu.

## 4.2.0 MAKOSA YA KIMOFOLOJIA NA KIMOFOFONEMIKI

Sehemu hii inahusu maumbo na miundo ya maneno. Kwa kawaida silabi ya kiswahili inaundwa kwa konsonati na vokali; ingawa mara nyingine konsonanti moja au vokali moja huenda ikaunda silabi. Kwa mfano katika neno 'mtolee' (m-to-le-e) kuna silabi nne konsonti ya kwanza [m] inaunda silabi moja ikiwa peke yake na vokali ya mwisho [e] pia inaunda silabi ikiwa peke yake. kutokana na tofauti za kimofolojia za lugha nyingi (taz. sehemu ya fonolojia katika sura ya tatu) silabi [m] hutamkwa [mu] na silabi [n] hutamkwa [in]. Haya ni makosa yanayoingiliana katika viwango vya fonolojia na mofolojia. Hata hivyo makosa ya kimofolojia tumeyaainisha hivi,

### 4.2.1. MABADILIKO KATIKA NGELI:

(a) kuongeza viambishi vya ngeli:

km:

| | | |
|---|---|---|
| makuku | - | kuku |
| manyumba | - | nyumba |
| matakataka | - | takataka |

Sentensi:

(i) "Makuku za kina Karuga zinaharibu 'Compound'" (Anna)

(ii) "Manyumba za Njiriri ziko mob (nyingi)" (Kariuki) kwa maana ya, "Njiriri ana nyumba nyingi"

(iii)Hisi matakataka simenjaa kila ma'ali." (Kimeu)

Makosa haya ya ngeli yanatokea katika majina ya ngeli ambayo hayana wingi (Taz. mifano hapo juu). Maoni yetu ni kwamba kwa kuwa wazungumzaji hawa wanafahamu kuwa majina ya kiswahili yanajipanga katika ngeli fulani za wingi na umoja, ndipo wanapochukulia kwamba majina hayo pia sharti yawe na wingi na umoja. Jambo jingine ambalo tumeligundua kutokana na uchunguzi wetu ni kwamba katika lugha za kwanza za wahusika hawa (Anna, Kariuki na Kimeu) majina pia hupangwa kufuatana na ngeli fulani za majina, na hii pia inaweza kuwa sababu mojawapo ya makosa kama haya ngeli kutokea ikiwa mhusika hafahamu kanuni za ngeli za majina ya kiswahili.

Mifano zaidi ya sentensi zilizo na makosa kama haya ya ngeli ni,

(iv) "Waria anachunga manyumba za juu (Mama Jane)

(v) "Wanatupanga matakataka yao hapa karibu". (Njeri)

(vi) "Wanauzanga mandizi tatu shilingi mbili" (Mwangi)

(b) <u>Kubadilisha kiambishi cha awali cha ngeli moja kwa kiambishi cha awali tofauti:</u>

<u>km</u>: "malisema" - walisema

"manakuja" - wanakuja

Sentensi: "Watu ma kajo (Council) marisema manakunja reo" (Mama Kamau).

Sentensi hii ina maana kwamba, "Watu wa 'Council' (Wafanyikazi wa 'City Council') walisema watakuja (tena) leo".

4.2.2 KUZUSHA VIAMBISHI VISIVYOKUWEPO:

(a) Kuzusha viambishi awali

km: "inchi" - nchi

"Umbu" - mbu

"Ongoja" - ngoja

Wavijana - vijana

sentensi:

(i) "Hii inchi imekuwa mbaya sana kwa waizi" (Odhiambo).

(ii) "Kunakuwaa na umbu nyingi sana usiku" (Kimeu)

(iii) "Tuliongocha basi paka saa tatu" (mama Jane).

(iv) "Wavijana ya chokoraa wanazungukazunguka kila pahali." (mzee Hassani).

Makosa ya kutamka 'inchi' badala ya 'nchi' na 'umbu' badala 'mbu' yanatokana na kule kutoweza kubainisha herufi moja kama silabi katika lugha ya kiswahili. Badala ya kutamka silabi [m] na silabi [n] pekee wahusika hawa ambao hawajamakinika katika matumizi ya lugha ya kiswahili wanafanya makosa ya kuzihusisha silabi hizi na vokali ili kuunda "silabi", ambazo zinaleta ukiushi dhidi ya lugha sanifu ya kiswahili. Hatukuweza kung'ammua moja kwa moja sababu za kuwepo kwa viambishi [o] katika neno 'ongoja' na [wa] katika neno 'vijana', Yamkini makosa haya yanatokana na athari za lugha mama; au inaweza kuwa ni makosa ya kianalojia ambapo mzee Hassan anajua kwamba ngeli ya majina ya watu (1/2) ni 'm' (katika hali ya umoja) na 'wa' (katika wingi).

km. 'mtu' - 'watu'

'msichana' - Wasichana', nk. kwa hivyo anaona kwamba hata 'kijana' wingi wake unaanza kwa kiambishi [wa], ndiposa badala ya kusema 'vijana' anaongezea kiambishi hicho cha [wa] na kuwa 'wavijana'.

(b) Kuongezea Kiambishi tamati kisichokuwepo

km: "tukanana" - tukana

"alisumbuana" - alisumbua

"nipatieko" - nipatie

"aliendako" - alienda

| | | |
|---|---|---|
| "imbanga" | - | imba |
| "pendanga" | - | penda |

Sentensi:

(i) "Watu ya kioski wanapendanga kutukanana sana". (Mwangi).

(ii) "Mtoto yake anasumbuanga. Analia saa yote" (Bi. Njuguna).

(iii) "Hebu nipatieko sabuni ya Omo" (Mama Shem).

(iv) "Fundi aliendako Taun (town)" (Lukalo).

(v) "Si mnaona vile kwaya inaimbanga msuri?" (Mama Rodah).

Uchunguzi umeonyesha kwamba makosa haya yanatokana na athari za lugha ya kwanza ambapo wazungumzaji huwa wana pachika viambishi tamati katika kiswahili" kulingana na miundo ya lugha zao za kwanza.

4.2.3 MAKOSA KATIKA MNYAMBULIKO WA VITENZI

(a) Kunyambua kitenzi kutokana na mzizi 'Pat-'

Km: pea - patia

Nipee - nipe (nipatie)

sentensi: (i) "Nimekupea 'change' yako" (Oduori).

(ii) "Nipee masiwa na mkati." (Anna)

(b) Makosa mengine ni kuhusu wiano wa kisarufi ambapo majina fulani hayatumiki kulingana na kanuni za kimofofonemiki. Kwa mfano, 'waizi" badala ya 'wezi' (wevi).

Sentensi: (i) "Waizi 'mezidi kufunja manyumba siku hizi." (Mzee Hassan).

Katika sentensi hii mzee Hassan hajafuata sheria za kimofofonemiki ambapo fonimu /a/ na /i/ huungana katika wiano wa kisarufi na kuwa /e/. Badala ya 'Waizi' neno likawa 'wezi'. Makosa haya yanatokana na ujuzi wa lugha katika kiwango cha kimsingi ambapo mzungumzanji anafahamu kwamba majina katika ngeli ya 1 na ya 2, huwa [m] katika umoja na [wa] katika wingi. Kwa hivyo kwa mzungumzaji huyu neno [mwizi] wingi wake ni [waizi].

(c) Makosa mengi zaidi yanahusu udondoshaj na uongezaji mofimu katika maneno yanayotamkwa na wahusika. Kwa mfano, tunapata sentensi kama hizi:-

<u>sentensi</u>: (i) <u>Sanyansanya</u> iyo bitu tufunge kasi." (Oloo).

Sentensi hii moja ina makosa katika viwango vya fonolojia, mofolojia na sintaksia. Katika upande wa mofolojia mhusika ametumia neno "Sanyasanya" badala ya 'kusanya' au 'kusanya - kusanya' '..iyo bitu ..' ina maana ya 'hivyo vitu' katika kiswahili fasaha. Kwa hivyo, mhusika alinuia kusema,

> "Kusanyakusanya hivyo vitu (ili) tufunge kazi." Miundo hii kiushi ya matumizi ya lugha aghalabu inatokana na kule kutomakinika katika matumizi ya lugha ya kiswahili na kutoifahamu miundo yake ya kisarufi, na pia athari za lugha ya kwanza kwani tofauti za kisarufi kati ya lugha hizi ndizo humwathiri mzungumzaji. Makosa mengine ya aina hii ni,

<u>Sentensi</u>: "<u>Mama</u> pana <u>sirika</u> biatu <u>tasona</u> tu". (Oloo)

Mzee Oloo hakuwa amevishona viatu vya mama mmoja katika wakati aliomuahidi, na mama alipokuja na kuvikuta viatu vyake havijashonwa Mzee Oloo alifanya ukiushi huu katika maongezi yake akijaribu kujitetea.

Kiambishi ambacho wahusika wengine wamependelea kukipachika katika vitenzi ambacho hakihitajiki mahali hapo ni kiambishi [ku]

(d) Matumizi ya kiambishi [ku -] jazilizi

sentensi: (i) :Alianiambia nikuje jana, kukuja sikumkuta.: (Njeri)

(ii)"Huyu mtoto hapedangi kukula chakula." (Anna)

Vitenzi vilivyopigwa msitari chini yake vinaonyesha kupachikwa kwa kiambishi [ku] na wazungumzaji kikiwa hakikuhitajika katika neno hilo. Aghalabu makosa haya yanatokana na athari za lugha za kwanza za wazungumzaji. Mzungumzaji anakiweka kitenzi katika ngeli ya (ku) ambapo haihitajiki.

Pia wazungumzaji wengine (mama vile mzee Hassan) wamependelea matumizi ya kuongezea [i] kuonyesha kitenzi kilichokamilika. Kwa mfano," anaunganisha [-na-] na [-i-] kwa maana ya kiambishi [-me-] cha wakati.

(e) Makosa katika matumizi ya viambishi vya wakati.

Sentensi: (i) Njiriri anaisha sema watu wasipitie kwake" (Mzee Hassan).

Sentensi: (ii) "Anakujanga kwa "saloon" kila mwezi" (Njeri) Neno "anakujanga" lina maana ya "huja", (mara kwa mara).

(iii)"Mtoto yake anasumbuananga sana" (Bi.Njuguna)

(iv) "siku hizi siendangi Marikiti, naendanga Korokocho." (Bi Maranya).

Makosa haya yanaonekana kuwa yanatokea katika matumizi ya vitenzi vinavyotokea "mara kwa mara", ambapo panahitajika kuwa na kiambishi [hu-] cha wakati au [ha] katika kukanusha. Ambapo Wazungumzaji wanaweka viambishi [-nga] au [-ngi] mwisho wa vitenzi kuonyesha wakati wa "mara kwa mara" katika hali ya kutendeka na kukanusha.

Tumejaribu kuorodhesha na kuelezea makosa ya kimofolojia na kimofofonemiki yanayotokea katika maongezi ya kila siku ya wahusika wetu. Haimaanishi kwamba makosa ya kimofolojia yanayotokea ni haya tu kati ya wakazi wa mtaa wa Kariobangi South bali huenda pakawa na mengine mengi ambayo yanaweza kujitokeza katika utafiti zaidi. Hata hivyo makosa mengine ya kimofolojia yameorodheshwa katika sehemu ya fonolojia kwa sababu pia yanaathiri matamishi makosa haya kama vile udondoshaji wa /m/ na /n/ katika miktadha ya /b/,/d/,/g/,/j/, na kadhalika. Kwa

mfano, 'imba' ikawa 'iba' kama tulivyoona katika sehemu ya fonolojia.

## 4.3 MAKOSA YA KISINTAKSIA

Makosa ya kisintaksia yanaambatana na yale ya kimofolojia ambapo wahusika wanatumia miundo ya kisarufi isiyo sawa kulingana na sarufi ya kiswahili sanifu. Kama tulivyokwishakuona katika sehemu za awali (km. 3.3.1.), ukiushi huu unatokana hasa na athari za lugha za kwanza (lugha ya mama) ya mzungumzaji. Baada ya kuzungumzia jinsi athari hizo zinavyoingilia matumizi ya lugha katika viwango vya kifonolojia na mofolojia, katika sehemu hii tunaorodhesha makosa tulivyoyapata kutokana na maongezi ya wahusika katika utafiti wetu. Makosa haya tumeyapanga katika visehemu mbalimbali.

(a) Makosa katika matumizi ya viashiria

km: "Hii" - huyu au hawa,

"Hizi" - haya au hivi

"Ile" - yule, wale, nk

Sentensi: (i) Hii mtoto amekufanana", (Muturi).

(ii)"Hii samaki ni "fresh" kweli?" (Akinyi)

Muturi na Akinyi hawakutumia viashiria sawa sawa katika sentensi hizi. Uchunguzi wetu umeonyesha kwamba makosa haya yanatokana na kule kutoifahamu miundo ya lugha barabara. Mzungumzaji hafahamu ni wapi atumie kiashiria gani. Hatofautishi kati ya upatanishi wa kisarufi katika ngeli mbali mbali.

Mifano zaidi ni,

(iii)"Hizi maji ni chafu." (Mary)

(iv) "Ulisoma hiyo kitabu?" (Oduor)

(v) "Ile mbusi ni ya Waria."(Kimeu).

Makosa haya pia yanatokana na sababu tulizozielezea zinazohusu viashiria katika makosa yaliyofanywa na Muturi na Akinyi.

Kama ilivyo makosa kuhusu viashiria, kuna makosa yanayolingana na hayo ambayo yanahusu matumizi ya vimilikishi.

(b) Makosa katika matumizi ya vimilikishi

km 'yangu' - wangu, na 'yake' badala ya wake

'yangu' - changu, vyangu, zangu.

'zangu - vyangu, na 'zake' - vyake.

Sentensi: (i) "mtoto yangu ni mkubwa." (Bi. Kipkorir)

(ii) "Nguo (wingi) yangu nilipeleka dobi." (Bi. Obiero)

(iii) "Kisu yangu iko kali sana" (Mzee Hassan)

(iv) "Hiyo ni viatu yangu, hebu shona haraka. (mama Jane).

Makosa haya, kama tulivyokwishaelezea hapo juu yanaombatana na yale ya kuhusu viashiria na sababu za kutokea kwa makosa haya ni hizo hizo kama tulivyokwisha kuzitaja.

(c) Makosa kuhusu idadi

km: 'mbili' - wawili, 'tatu' - watatu, n.k.

'mingi' - nyingi

Sentensi "Nataka samaki mbili." (Akinyi)

Sentensi: "Watoto yako ni tatu?" (Bi Kipkorir).

"Amebeba manguo mingi akapeleka dobi" (Bi. Maranya).

Makosa haya pia yanatokana na kutoufahamu upatanishi wa kisarufi katika lugha ya kiswahili. Kama tulivyokwisha kutaja katika utangulizi wa sura ya tatu, jinsi ngeli za majina zilivyoundwa katika lugha ya kiswahili haziambatani na mipangilio ya ngeli katika lugha zote za wahusika. Ni kwa sababu hii ambapo tunaona kwamba wazungumzaji wanafanya makosa kwa kutofahamu ni upatanishi gani wa kisarufi unaoambatana na ngeli fulani. Licha ya hayo, Bi Maranya amefanya kosa lingine la kudondosha neno "kwa" kabla ya neno 'dobi' katika sentensi, "Amebeba manguo mingi akapeleka dobi."

(d) Makosa Katika matumizi ya prepozisheni.

km: 'na' - kwa

'kwa' - (mahali isipohitajika)

Sentensi: (i) "Nilienda na miguu" (Kariuki)

(ii) "Kila siku anakujanga kwa dukani asubuhi." (Oduori)

(ii) "Akikuja piga yeye na mbakola." (Baba Mwangi).

Matumizi ya 'na' na 'kwa' huwatatanisha waongeaji wengine wa lugha ya kiswahili kutokana na kuathiriwa na lugha zao za kwanza. Kwa mfano, katika lugha ya kikuyu na kikamba (tulifanya uchunguzi) mtu akitafsiri moja kwa moja kutoka kwa lugha hizi atasema, 'kwenda <u>na miguu</u>" badala ya 'kwenda <u>kwa</u> miguu' kulingana na kiswahili. Ni athari kama hizi za tafsiri za moja kwa moja ambazo huleta ukiushi au makosa katika matumizi ya lugha. Makosa mengi kama haya katika upande wa wiano wa kisarufi ni katika sentensi,

(iv) "Alikwenda <u>kwa yeye</u> kumsalimia". (Bi. Nzioka)

Katika sentensi hii, '<u>kwa yeye</u>' ina maana ya 'kwake'. Mzungumzaji huyu ametumia muundo ulio sahili sana ambao unahusu kanuni za kimofofonemiki za wiano wa kisarufi. Hii ina dhihirisha kwamba mzungumzaji anaifahamu lugha katika kiwango cha chini ndiposa anatumia miundo kama hii. Tunapata mifano zaidi,

<u>sentensi</u>: (v) "Mitoto ile nakimbilia kwa mabarabara."
(Bw. Obiero)

(vi) "Mimi apana iko makosa. Ni "becos I was not aware"."
(Bw. Obiero)

(vii) "sisi bado ulisa wewe swali (Bw. Obiero)

Kama tulivyokwishataja katika utangulizi wa sura ya tatu, Bw. Obiero anakifahamu Kiswahili kwa kiwango kidogo sana na mara nyingi hutumia lugha ya kiingereza au kuchanganya Kiswahili na kiingereza katika mazungumzo yake. Yeye mwenyewe, amewahi kukiri kwamba haipendelei lugha ya kiswahili na anaelekea kwamba hii ni sababu moja ya kutojishughulisha kwake kuzingatia miundo inayofaa katika matumizi yake ya lugha hii.

Makosa mengine yanayohusu miundo ya kisintaksia ni,

<u>Sentensi</u>: (i) "Yeye lingia kwa bas na kupatiana siling sirini."(Onyango)

(ii) "Ghwishatuma yeye ndukani."(mama Kamau).

(iii) "Pea mimi chembe yako, nataka lima kwangu."(Mama Jane).

(iv) "Sikukuwa ninajua."(Mary)

## 4.4 HITIMISHO

Makosa haya ya kisintaksia ambayo tuliyapata kutokana na utafiti wetu tumeona kwamba licha ya kuwa yanatokana na athari za lugha za kwanza ni kwa sababu mara nyingi wazungumzaji pia hawaifahamu barabara miundo ya kisarufi ya lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hii wanatafsiri moja kwa moja sentensi kutoka katika lugha zao za kwanza, ambapo ikiwa miundo ya lugha zao haifanani na miundo ya sentensi za Kiswahili makosa (ukiushi) hutokea katika maongezi yao.

Tumekwishasema pia kwamba haitawezekana kuorodhesha na kuainisha aina zote za ukiushi wa kisintaksia katika miktadha mbalimbali. Tunalofanya ni kutoa mifano michache inayoonyesha makosa mbalimbali yanayofanyika katika viwango mbalimbali tulivyovitaja katika kuiwasilisha kazi yetu ya utafiti.

Baada ya kuzungumzia hoja katika viwango vya kimofolojia na kisintaksia, katika sura ifuatayo tutazijadili hoja kuhusu semantiki na leksia kama zilivyojitokeza katika utafiti wetu.

# SURA YA TANO

## 5.0 UKIUSHI WA KIMSAMIATI

## 5.1 UTANGULIZI

Tumekwisha kuyaelezea madhumuni yetu katika sura ya kwanza, sehemu ya 1.2 kwamba, katika kulishughulikia swala la ukiushi unaotokana na matumizi ya msamiati, tutakuwa kwa hakika tukizijadili hoja zinazohusu leksia na Semantiki.

Katika utafiti tulioufanya katika mtaa wa Kariobangi South, mjini Nairobi, makosa yaliyojitokeza kwa upande wa semantiki na leksia katika maongezi ya wahusika, yalitokana sana na uingizaji wa msamiati wa lugha za kwanza katika Kiswahili. Wahusika wanazitaja dhana fulani na kuyataja majina fulani kwa lugha zao za kwanza kana kwamba hazina msamiati wake katika kiswahili. Kwa mfano, bidhaa zinazouzwa sokoni kama vile 'mbaazi', 'mboga za mchicha' na 'maparachichi' wanaziita "njughu", "terere" na "makorovia". Uchunguzi wetu umetuelekeza kung'amua kwamba sababu zenyewe zatokana na kule kutoufahamu msamiati unaopaswa kutumika na si kwa sababu ya athari za lugha za kwanza tu.

Makosa mengine yanahusu matumizi ya msamiati wa lugha ya kiswahili lakini kwa maana isiyokusudiwa. Kwa mfano katika kiswahili sanifu, maana inayotokana na dhana, "mama-watoto" ni kwamba ni "mzazi wa kike". Katika kuufanya

utafiti wetu tumegundua kwamba kuna watu wanaotumia dhana hiyo wakimaanisha "bibi" au "mke" kwa jumla hata kama hajapata watoto. Kwa mfano, mhusika wetu mmoja (Lukalo) alimtaja mchumba wake, ambaye hata hana mtoto, akisema. "Huyu ni mama watoto wangu." Lukalo mwenyewe pia alikiri kwamba hata hana watoto bado. Alitumia "mama watoto" akimaanisha mke (atakayemuoa).

## 5.2 MISAMIATI ISIYOKUWA YA KISWAHILI

Misamiati ambayo si ya kiswahili inayotokana na maongezi ya wahusika wetu imegawanyika mara mbili. Kuna misamiati ambayo ni maneno ya lugha ya kiingereza na ile ya lugha za kwanza za wahusika. Katika utafiti wetu tumepata matumizi ya maneno ya kiingereza yanayoingizwa katika sentensi za lugha ya kiswahili. Kwa mfano:-

(i) "Hii samaki ni "fresh" kweli?" (Akinyi)

(ii) "Nimegunduako 'style' mpya ya kufunga "piece"." (Mary).

(iii) "Ni becos I was not aware." (Bw. Obiero).

Kama tulivyokwishakuelezea katika sura ya tatu sehemu ya 3.1, Bw. Obiero hakifahamu kiswahili barabara na mara nyingi hutumia miundo ya kiingereza katika sentensi zake au kuyapachika maneno ya kiingereza. Lakini katika

"ukiushi" uliofanywa na Akinyi na Mary tumeona kwamba licha ya kuwa ni kutokana na athari za matumizi ya lugha ya kiingereza, pia ni kwa sababu ya kutoimudu lugha kikamilifu ndivyo wanavyotumia msamiati wa kiingereza katika sentensi zao. Tuliwahoji baada ya kumaliza kuichukuwa data yetu ikiwa wanafahamu msamiati wa kiswahili wenye maana ya 'fresh', 'style' na 'piece' na tukagundwa kwamba hata hawaufahamu. Tumeona pia kwamba maneno haya yanatumika sana jinsi yalivyo, katika kiswahili cha wakazi wa mataa wa Kariobangi South.

Msamiati mwingine unahusu maneno yanayotoka katika lugha za kwanza, km:

(i) "Kilo ya mbosho ni silingi kumi na tano"(Mama Wambua)

(;Mbosho" ina maana ya maharagwe)

(ii) "Siku hizi wanausanga 'karoti Kifago moja rufia" (Bi. Njuguna)

'Kifago' ni fungu la vitu vinavyopangwa sokoni, na 'rufia' ni shilingi mbili.

Mananeno haya yanayotokana na msamiati wa Kikuyu yanatumika baina ya wakazi wa Mtaa wa Kariobangi South na kueleweka kana kwamba hapana msamiati wake badalia katika lugha ya Kiswahili.

## 5.3. MSAMIATI WA KISWAHILI AMBAO HAUKUTUMIKA KWA MAANA YAKE HALISI

Licha ya kwamba wahusika wametumia misamiati kutoka katika lugha za kwanza na kuiingiza katika kiswahili, tumepata pia, matumizi ya maneno ya kiswahili ambayo, kulingana na muktadha ambapo yametumika, maana yake halisi haijitokezi. Kutokana na utafiti wetu, tumeona kwamba, maana ya neno kijana, kwa mfano, ambayo ni mtoto mwanamke au mwanamume ambaye hajafikia kuwa mtu mzima, hajitokezi hivyo kulingana na jinsi neno hilo linavyotumiwa katika sentensi hii;

(i) "Anasoma kwa shule ya vijana na Wasichana". (Kariuki)

Tunaona kwamba Kariuki alichukulia kwamba vijana ina maana ya wavulana pekee. Hii ni aina moja ya ukiushi katika upande wa msamiati na maana.

Mifano mingine zaidi ni,

(ii) "Alitoka asubuhi juu hakutaka kuchelewa" (Njeri)

(iii) "Bado sijaosha nyumba yetu"(Anna).

(iv) "Chukuwa basi ya Ndandora". (Peter)

Katika mfano wa (ii) Njeri amelitumia neno 'juu' kwa maana ya 'kwa sababu'. Msamiati huu unatokana na athari za kisheng ambapo neno hili hutumika sana. Anna naye ametumia neno 'kuosha' kwa maana ya 'kusafisha'. 'Kuosha' nyumba kunaashiria kule kuisafisha kuta, milango na madirisha ambapo katika mukadha wa matumizi ya msamiati huu katika sentensi mzungumzaji alikuwa anawasilisha maana ya kusafisha sakafu ya nyumba yao. Uchunguzi umeonyesha kwamba kosa hili latokana na athari za lugha ya kwanza ya mzungumzaji. Mfano mwingine zaidi ni:-

(v) "Chukua basi ya namba 'Twenty Three'" (Mama Jane)

Muundo wa kisarufi na msamiati aliotumia mama Jane unaonekana kuwa na athari za lugha ya Kiingereza. Kwa mfano neno 'chukua' katika muktadha huu lina maana ya "take" katika Kiingereza,

"Take bus number twenty three."

Msamiati mwingine unaotokana na neno la kiswahili 'chokora' ni 'chokoraa' ambalo limetumika kwa maana ya 'manamba' na 'jaa' katika sentensi ifuatayo:-

(vi) "Matakata hizi zimejaa kwa <u>chokoraa</u>. <u>Machokoraa</u> watakuja kuokota makaratasi." (Mwangi) Labda msamiati huu umetokana na tabia ya manamba ya kuchokora-chokora kwenye majaa wakitafuta riziki.

(vii) "<u>Umekaranga</u> chakula na mafuta mengi" (Bi. Maranya) Kwa kufahamu kiswahili haba, Bi. Maranya anatumia neno 'karanga' kwa maana ya 'kaanga'. Neno 'karanga' limo katika msamiati wa kiswahili lakini kwa maana tofauti kabisa kulingana na jinsi linavyotumiwa. 'Karanga' ni 'njugu' kwa kiswahili.

Neno lingine la kiswahili ambalo halitumiwi kwa maana yake halisi ni 'kupatiana' ambalo katika kiswahili lina maana ya 'kumpa mtu (kitu) na yeye akupe au ampe mwingine'. katika sentensi,

(viii) "Njoroge ni mtu mbaya, hawezi <u>kupatiana</u> kitu." (Bw. Onyango)

Onyango ana maana kwamba Njoroge ni mchoyo, hampi mtu kitu chake. Kwa hivyo, kulingana na maana halisi ya neno hilo, halikutumika kisawasawa katika sentensi hiyo. Inaelekea kwamba Onyango aliuiga msamiati huo kikasuku kutokana na wazungumzaji wa asili ya Kikuyu kwa sababu hii

inaonekana kuwa na athari za lugha hiyo ambapo neno la "kumpa" lina maana sawa na kupatiana.

## 5.4. TAFSIRI ZA MOJA KWA MOJA KUTOKANA NA LUGHA ZA KWANZA

Kwa mtu ambaye haifahamu lugha kikamilifu mara nyingi anatafsiri maneno kutoka katika lugha yake ya kwanza na kuyaingiza katika lugha ya pili. Kwa mintarafu ya utafiti wetu, wahusika walifanya makosa haya:-

(i) "Watoto na ni wadogo Wanakunywa sigara." (Mama Roda)

(ii) "Nimwagie chai kwa hii kikombe" (Mama Shem).

(iii) "Mimi sipendi kulea mtoto saa yote" (Mama Shem).

(iv) "Waria anachunga manyumba za njuu." (Kimeu)

(v) "Anagoja mtoto wa dada yake" (Akinyi).

Maneno haya yaliyopigiwa mistari yanatokana na tafsiri za moja kwa moja kutoka katika lugha za kwanza za wazungumzaji. Uchunguzi wetu umedhihirisha kwamba lugha ya Kikuyu haitofautishi kati ya "Kunywa" na "kuvuta". Ndiposa, mama Roda anafanya makosa ya kutokuweza kubainisha tofauti katika maneno haya katika lugha ya kiswahili. Ni sawa katika Kikuyu mtu kusema, "kunywa sigara."

Katika Kibukusu, tumeona kwamba "kumwaga chai" ina maana ya moja kwa moja ya "kutia chai" kwa hivyo Mama Shem ametafsiri kutoka kwa lugha yake ya kwanza anaposema hivyo. "Kulea mtoto" pia inatokana na sababu kama hizo. Maana yake ni "kumpakata mtoto".

Katika ukiushi anaoufanya Kimeu, "Kuchunga" amelichukulia kwa maana ya "Kulinda". Naye Akinyi anatumia neno "ngoja" kwa maana ya "angalia" au "linda". Kama tulivyosema makosa haya yanatokana na tafsiri za moja kwa moja kutoka lugha za kwanza.

## 5.5. HITIMISHO

Tumeyapanga makosa ya msamiati katika sehemu tatu. Makosa yanayoyokana na matumizi ya msamiati usiokuwa wa kiswahili, makosa yanayoyokana na msamiati wa kiswahili ambao haukutumika kwa njia inayopasa, na makosa yanayotokana na tafsiri kutoka lugha za kwanza.

Kila lugha ina msamiati wake, kwani msamiati unahusu jumla ya maneno yanayopatikana katika lugha. Kwa sababu ya maingiliano kati ya wanadamu na kupatikana dhana mpya, lugha 'hukopa' au pia 'kubuni' msamiati mpya ili kukabiliana na mabadiliko hayo. Ni wazi kwamba dhana fulani inaweza kuwa na msamiati ambao haupatikani katika lugha nyingine. Jambo hili latokana hasa na tofauti za kitamaduni na kimazingira.

Tumeona kwamba ikiwa lugha anayoizungumza mtu kama lugha yake ya kwanza ina upungufu fulani wa msamiati wa lugha ya pili, mzungumzaji anaweza akatatizika katika matumizi ya msamiati huo hata asiutumie kwa njia sawa.

Pia kutomakinika katika matumizi ya lugha fulani au kuifahamu lugha 'nusu-nusu' husababisha mzungumzaji akatumia msamiati wa lugha yake na kuuingiza katika lugha ya pili na kusababisha ukiushi. Pia tumeona kwamba wahusika wengine wametumia misamiati fulani ya kiswahili kwa maana tofauti kabisa na ile inayokusudiwa.

## SURA YA SITA

## 6.0. HITIMISHO

Katika sura ya kwanza sehemu ya 1:2 tulisema kwamba tulidhamiria kuangalia matumizi ya lugha na ukiushi unaojitokeza dhidi ya lugha sanifu. Tulilenga kuonyesha makosa (ukiushi) yanayotokea katika maongezi ya wahusika katika utafiti wetu. Makosa hayo tumeyaainisha katika viwango vya fonolojia, sarufi (mofolojia na sintaksia) na semantiki na leksia. Pia tumejaribu kutoa maelezo na sababu zinazoleta makosa hayo kulingana na utafiti tuliolufanya katika mtaa wa Kariobangi South, mjini Nairobi.

Kwa minajili ya utafiti wetu ukiushi wa kifonolojia unatokana na athari za lugha za kwanza ambapo baadhi ya sauti kama vile /l/ na /r/ hazipatikani katika lugha za kwanza za wazungumzaji wengine. Kwa mfano, tumeona kwamba kwa sababu ya ukosefu wa sauti /l/ katika lugha ya Kikuyu wazungumzaji wengi wanaozungumza lugha hii kama lugha yao ya kwanza wanatatanishwa na matumizi ya /l/na/r/. Sauti hizi zinajuzolikana kama 'likwidi' (liquids) katika taaluma ya ismu kutokana na sifa za kifonetiki. Kwa hivyo makosa ya kimatamshi yametokana sana na athari za lugha za kwanza kuliko mazingira. Labda ni kwa sababu ya 'Accommodation Model' (Grimshaw, 1967) ambapo tumepata wazungumzaji wawili

(Mary ambaye ni Mluhya na Mama Jane ambaye ni Mteso) wakifanya makosa ya kimatamshi kwa kutofatautisha kati ya /l/ na/r/ walipokuwa wakizungumza na wazungumzaji wengine wa asili ya kikuyu wakiwa katika miktadha tofauti.

Katika kiwango cha sarufi, ukiushi umetokana hasa na tofauti za kimofolojia na kisintaksia kati ya lugha za kwanza na kiswahili. Hoja hii imejidhihirisha katika matumimizi ya sintaksia katika upatanisho wa ngeli ambapo lugha nyingine (kama vile Kijaluo, Kiteso na Kinandi) haziainishi ngeli kuambatana na mbinu zinazotumika katika kiswahili na lugha za Wabantu zilizotajwa katika utafiti. Makosa ya kisarufi yanatokana na kutojua jinsi ya kuyapanga majina katika ngeli za kiswahili na pia kulingana na upatanisho wa kisarufi katika sentensi.

Katika kiwango cha leksia na semantiki tunapata matumizi ya msamiati wa kiingereza na matumizi ya maneno ya lugha za kwanza. Tumeona kwamba kiwango cha elimu huenda kikamuathiri mtu katika matumizi ya lugha. Kwa mfano mtu mwenye shahada ya chuo kikuu akiwa hana udhati na lugha ya kiswahili na labda anaidharau, anafanya makosa yanayotokana na athari za kiingereza kuliko yule ambaye hata hajafika katika shule ya upili. Hata hivyo mara nyingi ni vigumu kujua ikiwa mzungumzaji amekosa kisawe cha neno la kiswahili au amefanya kusudi kwa kutumia neno la kiingereza

au la lugha yake ya kwanza. Katika mazungumzo tuliyoyarekodi hatukuweza kung'amua sababu kwa hivyo tuliyaorodhesha makosa hayo kama ukiushi kwani lengo letu lilikuwa ni kuchunguza lugha katika kiwango cha 'utendaji' na wala sio katika kiwango cha 'ujuzi'.

Makosa mengine yanatokana na kule kutomakinika katika matumizi ya lugha na msamiati wake. Kwa mfano mzungumzaji anapotaja 'ndizi' kwa maana ya 'mgomba' yamkini ni kwa sababu ya kutoufahamu msamiati sawa wa kiswahili.

Msimamo wa mtu kuhusu lugha ya kiswahili huathiri matumizi yake ya lugha hiyo. Mtu ambaye hakipendi, au anakidharau kiswahili anaonekana kufanya makosa mengi zaidi hasa ya kileksia na kisintaksia, kama ilivyodhihirika katika utafiti wetu. Kwa mfano, katika kuufanya utafiti huu tumeona kwamba, Bwana Obiero (ambaye ni Meneja katika kampuni), na mke wake walionyesha kutokipenda kiswahili na wakakiri jambo hilo. Kiswahili chao wanachokifahamu walisema ni 'kiswahili moja - moja'. (Taz. sura ya tatu sehemu ya 3.1.2).

Jambo lingine ambalo tumeweza kuling'amua kutokana na utafiti wetu ni kwamba wazungumzaji wengine (Kama vile Binti Obiero mweye umri wa miaka 21 na Njeri mwenye umri wa miaka 19) wamependelea matumizi ya 'lugha ya kimtaa' katika

mzungungumzo yao. Hii ni lugha wanayojifunza 'kikasuku' huko mitaani ambayo tayari ina ukiushi mwingi dhidi ya lugha sanifu. Kuna maneno na miundo ya 'kisheng' katika lugha hii hasa wanapozungumza na wenzao ambao ni marika. Hoja hii aghalabu imejikita katika <u>'Accommodation Model'</u> (Grimshaw, 1967) ambayo tumekwisha kuitaja hapo awali. Kwa hivyo tunaweza kutoa kauli ya jumla kwamba kuna ukiushi unaojitokeza kulingana na muktadha na sajili. Kwamba, mzungumzaji mmoja anaweza kujitokeza na 'vilugha' tofauti kulingana na yule anayezungumza naye, wakati gani na kuhusu nini.

Kwa minajili ya utafiti wetu, hapana mashiko kwa dai kwamba kiswahili cha ya sehemu ya Kariobangi South ni cha aina moja. Ukiushi unaojitokeza si ukiushi unapatikana baina ya wazungumzaji wote bali kila mzungumzaji ana ukiushi (mtindo) wake binafsi. Kama anavyosema Buffon (1763), "Mtindo ni mtu mwenyewe". Ndiposa, kama tulivyokwishataja katika sura ya tatu sehemu ya 3:1:2 kuna misemo ya 'Kuongea kiswahili kama Mjaluo," "Kuongea kiswahili kama Mkikuyu", na kadhalika.

Katika utafiti huu hatukuzingatia hoja kuhusu kiimbo na mkazo (msistizo). Hii ni kwa sababu ingehusu kazi nyingi sana na ujuzi mwingi wa taaluma inayohusu mambo ya kiimbo na mkazo. Haya hatungeweza kuyafanya kikamilifu

tukizingatia kwamba tumebanwa katika kipindi fulani cha wakati wa kuikamilisha na kuiwasilisha kazi hii. Jambo jingine pia muhimu kutaja ni kwamba hatukuzingatia pragmatiki ambayo hujitokeza katika viwango mbalimbali. Kutozungumzia swala la pragmatiki vilevile kumetokana na sababu kwamba muda pia haungeturuhusu kuweza kuikamilisha kazi hiyo yote. Kuzichukuwa nyanja zote zinazohusu lugha na kuzijadili katika kazi moja ni jambo ambalo kwa kweli haliwezekani kufanywa na mtu mmoja katika kipindi kimoja, fauka kipindi cha miezi minne.

Hata hivyo vile vipengee vya lugha tulivyovizingatia na mitazamo tuliyoitumia kama misingi yetu ya nadharia imefaa sana katika kulitafiti na kulifikia lengo letu.

## 6.1. MAPENDEKEZO

Kama tulivyokwishataja hapo awali (sura ya kwanza) sifa mojawapo ya lugha iliyo hai (na pana) ni kule kuwa na makosa yanayofanywa mara kwa mara. Kwa hivyo shughuli za uchunguzi wa lugha hiyo ni za kudumu kwa wakuzaji wa lugha na kwa jumla wazungumzaji wa lugha ya kiswahili. Jones, R. R. (1973) amegundua kutokana na utafiti wake kwamba nchi ambazo zimefanya usanifishaji wa lugha zao (rasmi na za kitaifa) hupata ufanisi zaidi katika maendeleo yao ya kiuchumi kuliko nchi ambazo hazijasanifisha lugha zao.

Yafaa kulizingatia sana jambo hili kulingana na lugha yetu ya kiswahili; tujaribu kutathimini jukumu la kiswahili katika maendeleo ya Taifa letu. Inapasa pia, katika utafiti kama huu, mtafiti achukuwe angalau kipengee kimoja na kukitafiti vilivyo. Kwa mfano 'Ukiushi katika kiwango cha fonolojia' au 'Ukiushi katika kiwango cha sintaksia', na kukishughulikia kwa marefu na mapana yake kwa muda unaofaa. Nyanja nyingine ambayo hatukuishughulikia hapa ni kuhusu kiimbo na msistizo (au mkazo). Mtafiti anaweza kuyashughulikia mambo haya mawili pekee na kujijokeza na mwongozo mwafaka kuhusu matumizi ya Kishwahili.


Hatimaye wapenzi na watumizi wa kiswahili wajitahidi kujifunza na kukitumia kiswahili fasaha na kujivunia lugha yao. Kama anavyosema Jones (1973), labda kwa kufanya hivyo tunaweza kuharakisha maendeleo ya nchi yetu.

## MTAA WA KARIOBANGI SOUTH




Ramani haikuchorwa kwa vipimo maalum

KIJALIZO:



Kanisa

Stesheni ya petroli

Vibanda vya Juakali

Nyumba

Eneo la Mtaa wa Kariobangi South

# MAREJEO


Bailey, C. J. N., (1973) Variation and Linguistic Theory. Arlington, Va. Center for Applied Linguistics.

Cazden, C. B., (1967), `On Individual Differences in Language Competence and Performance' J. Spec. Ed. Vol. 1, UK. 135-150.

Chambers, J. K. na Trudgill, P., (1980) Dialectology Cambridge: Cambridge University Press.

Cheshire, J., (1982), Variation in an English Dialect: A sociolinguistic Study. Cambridge University Press.

Chiraghdin, S. na Mnyampala, M. (1977), Historia ya Kiswahili. O.U.P. Nairobi

Duran, J. J. (1975), The Role of Swahili in a multi-lingual Rural Community in Kenya. Tasnifu ya PhD. SANFORD UNIVERSITY.

Doughty, P., (et al), (1972) `Participation in conversation: The Phenomenon of Response Matching. Karatasi iliyosomwa katika mkutano wa kila mwaka wa 'Social Psychology Section of the British Psychological Society. BRIGHTON.

Fishman, J.A., (1966), Language Loyalty in the United States. The Hague. MOUTON.

Giles, H., na Powesland, D. F., (1975) Speech Style and Social Evaluation. Academic Press. LONDON.

Gile, H., na St. Clair, R. (Waha), (1979), Language and Social Psychology. Oxford. BLACKWELL.

Gilman, C. (1976) `Lexical Reinterpretation in Zairean Swahili', Katika jarida la Kiswahili, Tol. 46/2 Sept. 1976. Mbughuni, K. (et al) (Waha) CHUO KIKUU CHA DAR-ES-SALAAM.

Gumperz, J. J. (1977), Language in Social Groups SANFORD UNIVERSITY PRESS; SANFORD. CALIFORNIA.

Halle, and Stevens (1964),

Homans, G. C. (1961), Social Behaviour. Harcourt, Brace and World. NEWYORK.

Hymes, D. (1967), 'Models of the Interaction of Language and Social Setting'. Journal of Social Issues, Vol. 23/2. uk. 8-28.

Jones, R. R. (1973), `Linguistic Standardization and National Development'. Internationa Journal of Psychology. uk. 51-54.

Labov, W. (1970), "The Logic of Non-standard English" in Monograph Series on Language and Linguistics James, E. A., (Mha.) No. 22. Georgetown University.

Labov, W. (1970), `The Study of Language in its Social Context'. Studium Generale, Vol. 23. uk. 66-84.

Labov, W. (1966), The Social Stratification of English in New York City. Washington DC. Center for Applied Linguistics.

Labov, W. (1968), "A study of the Non-standard English of Negro and Puerto Rican Speakers in New York City". Vol. I na II. Final Report, Cooperative Research Project 3288. Washington DC., US Office of Health, Education and Welfare.

Le Page, R. B. (1968), The Problem of Description in Multilingual Communities. Transanctions of the Philological Society. uk. 189-212.

Lyons, J. (1968), Introduction to Theoretical Linguistics. Cambridge University Press. Cambridge.

Macaulay, R.K.S. (1977), Language, Social Class and Education. Edinburgh. Edinburgh University Press.

Markova, I. (1978),(Mha.) The Social Context of Language. John Wiley and Sons. CHICHESTER.

Mbaabu, I. (1978) Lugha ya Kiswahili. Kenya Literature Bureau. NAIROBI.

Milroy, L. (1980) Language and Social Networks. Oxford. Blackwell.

O'Donnell, W. R. na Todd, L. (1980), Variety in Contemporary English. LONDON. George, Allen and Unuin.

Petyt, K. M. (1977), `Dialect and Accent in the Industrial West Riding: a Study of the Changing Speech of an Urban Area'. PhD. Thesis. University of Reading.

Pugh, A. K. (et al), (1980), _Language and Language Use_.

Quine, W. V., (1953), _From A Logical Point of View_. HARVARD UNIV. PRESS. CAMBRIDGE. MASSACHUSSETTS.

Quirk, R. (1966), "Acceptability in Language", Proceedings of the University of New-Castle-upon -Type Philosophical Society Vol. 1, No. 7. uk. 79-92.

Reid, E. (1978), "Social and Stylistic Variation in the Speech of Children: Some evidence from Edinburgh". P. Trudgill (Mha.), _Sociolinguistic Patterns in British English_. uk. 158-171. LONDON. Edward Arnold.

Romaine, S. (1975), `Linguistic Variability in the Speech of Some Edinburg School Children'. M. Litt. Thesis. University of Edinburgh.

Rosen, H. (1972), _Language and Class: a Critical look at the Theories of Basil Bernstein_. Bristol: Following wall Press.

Sapir, E. (1921), _Language: An Introduction to the Study of Speech_. A Harvest Book. NEW YORK.

Saussure, de F. (1966), _Course in General Linguistics_. (Waha.) C. Bailey and Albert Sechehaye. McGraw-Hill Book Company. NEW YORK.

Thakerar, J. N. (et al), (1982), `Psychological and Linguistic parameters of Speech Accommodation Theory'. Ktk. Advances in the Social Psychology of Language C. Fraser and K. R. Scherer (waha.) Cambridge. Cambridge University Press.

Trudgill, P. (1974), The Social Differentiation of English in Norwich. Cambridge. Cambridge University Press.

Trudgill, P. (1974), Sociolinguistics: An Introduction. Penguin Books. LONDON.

Trudgill, P. (1978), (mha.), Sociolinguistic Patterns in British English. LONDON. Edward Arnold.

Van Dijk, T. A. (1975), Recalling and Summerising Complex Discourse. University of Amsterdam Mimeo. Dept. of General Literacy Studies.

Wakelin, M. F. (1972), English Dialects. An Introduction. Athlone Press. LONDON.

Weinreich, U. (1953), Languages in Contact, Findings and Problems. New York. Linguistic Circle of New York.

Whorf, L. B. (1956), `Selected Writings', in Carroll, J. B., (mha.). Language, Thought and Reality. The M.I.T. Press. Cambridge. MASSACHUSSETTS.

Wolfram, W. (1969), A Sociolinguistic Description of Detroit Negro Speech. Washington DC: Center for Applied Linguistics.

Wolfram, W. na Fasold, R. W. (1974) *The Study of Social Dialects in American English Englewood Cliffs* N. J., Prentice - Hall.

Wolfson, N. (1976), "Speech Events and Natural Speech: Some Implications for Sociolinguistic Methodology". Katika *Language in Society* - 512 uk. 189-209.